epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Oktoba 3, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581818
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**FERNANDES AFUTIWA KADI NYEKUNDU**

UKURASA WA 4

**MCHUNGAJI MATATANI, ADAIWA KUENDESHA MAOMBI CHONGANISHI**

UKURASA WA 5


**WANASHERIA 'SAUZI', UINGEREZA KUMSAIDIA KABENDERA RUFANI DHIDI YA VODACOM**

UKURASA WA 12

**MABINGWA MUHIMBILI WANAVYOVUNA NYWELE NA KUOTESHA KWENYE KIPARA KAMA MPUNGA**

# Mtaalamu atoa angalizo matumizi dawa ya meno

• **Ataja** kiwango kinachotakiwa kwenye mswaki kulingana na umri... *Endelea ukurasa wa 2*



*"Kwa wenye miaka mitatu hadi mitano, weka dawa ya meno kwa ukubwa wa punje ya harage 9900-1000 ppmF-Dawa ya meno maalumu kwa watoto). Miaka sita mpaka umri wa mtu mzima, weka dawa ya meno ijae eneo lote la brashi ya kwenye mswaki (1400-1500 ppmF-dawa ya meno ya watu wazima).*

# CHADEMA yamkana aliyetoa kauli ya udini

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

# Gesi yageuka mateso kwa madereva magari, bajaji

UKURASA 3



Bajaji zinazotumia gesi, zikiwa kwenye foleni ya kujaza nishati hiyo, katika eneo la Uwanja wa Ndege, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**MICHEZO** **YANGA PRINCES, JKT FAINALI NGAO YA JAMII** UK.23 **KATUNI** UK.6

## Keissy aonesha nia ya kurudi bungeni

**Mussa Mwangoka,** MPANDA

MWANASIASA machachari na aliyewahi kuwa Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Ally Keissy, ameonyesha nia yake ya kugombea tena ubunge katika jimbo hilo baada ya kuangushwa mwaka 2020.

Keissy amesema dhamira yake ya kugombea ubunge kwenye jimbo hilo iko pale pale licha ya jimbo hilo kuongozwa na mbunge kutoka upinzani.

Katika kinyang'anyiro cha uchaguzi mkuu wa mwaka 2000, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilipoteza kiti cha ubunge katika jimbo hilo baada ya mbunge wa sasa, Aida Khenan, kumbwaga Keissy aliyekuwa katika kwenye nafasi hiyo kwa vipindi vitatu mfululizo.

Akizungumza kwa njia ya simu jana kutoka Sumbawanga mkoani Rukwa, Keissy alisema nia yake ya kugombea ubunge kwenye jimbo hilo haijabadilika kwa kuwa haoni kitu kipya kinachofanywa na mbunge wa sasa.

"Nataka kurudi kugombea kwa kuwa mbunge aliyepo hivi sasa hakuna cha tofauti alichofanya. Nilikuwa nimebuni miradi mingi ya maendeleo kwa wananchi wa Nkasi Kaskazini lakini michache tu ndiyo ametekeleza na mingine bado. Kero bado ni nyingi, hivyo kuna umuhimu wa kurudi tena," alisema.

Hata hivyo, alipotakiwa kutoa ufafanuzi ni miradi ipi ambayo mbunge wa sasa ametekeleza, hakuwa tayari kufanya hivyo, badala yake alieleza nia yake ni kugombea tena ubunge ili kutatua kero za wananchi ambazo ni ukosefu wa maji safi na salama na barabara za vijijini.

Hadi sasa, Jimbo la Nkasi Kaskazini linaonekana kuwa lulu kwa wana CCM wengi wanaonyemelea kugombea ili kumng'oa Kenani. Hadi sasa kuna watu takriban 20 wanatajwa kuwania jimbo hilo akiwamo Mwenyekiti wa zamani wa CCM Mkoa wa Rukwa, Rainer Lukara.

Khenani alishinda ubunge baada ya kupata kura 21,226 na kumshinda Keissy wa CCM ambaye alipata kura 19,972.

Keissy anakumbukwa kwa matukio kadhaa akiwa bungeni likiwamo la kunusurika mara mbili kupigwa na wabunge wa Zanzibar, huku wakimtolea lugha za kejeli na matusi.

Keissy aliwahi kujenga hoja akieleza udhaifu wa katiba ya nchi katika suala la Muungano baada ya kutoa maneno yaliyodaiwa kuwa ya kashfa kwa wabunge wa Zanzibar wakati wa akichangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Tukio lingine ni wakati wa vikao vya Bunge Maalumu la Katiba. Alinusurika pia kupigwa baada ya kupinga Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Muungano.

Akichangia mjadala wa Katiba, mbunge huyo asiyeisha vituko, alisema haiwezekani Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Muungano kwa kuwa hakuchaguliwa na wananchi wa Tanzania Bara jambo lililozua tafrani bungeni.

# Mtaalamu atoa angalizo kiwango cha matumizi ya dawa ya meno

**Na Christina Mwakangale**

MATUMIZI sahihi ya kiwango cha dawa ya meno kwenye mswaki, kabla ya kuswaki kinywa ni chanzo cha kuyakinga dhidi ya kuoza na kutoboka, imeelezwa.

Aidha, ubora wa dawa za meno zenye madini ya floridi, umeelezwa kuongeza ulinzi wa meno kwa kuyakinga dhidi ya kuoza.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Kinywa na Meno katika Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, aliyasema hayo, hivi karibuni wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii.

Alisema ili kujikinga na meno dhidi ya kuoza, inashauriwa kupiga mswaki meno mara mbili kwa siku (asubuhi na usiku kabla ya kulala) kwa kutumia dawa yenye madini ya floridi iliyo na ubora.

"Kuanzia jino la kwanza linapoanza kuota na hadi miaka miwili, weka dawa ya meno kwa ukubwa wa punje ya mchele (900-1000 ppmF-Dawa ya meno maalumu kwa watoto).

"Kwa wenye miaka mitatu hadi mitano, weka dawa ya meno kwa ukubwa wa punje ya harage 9900-1000 ppmF-Dawa ya meno maalumu kwa watoto). Miaka sita mpaka umri wa mtu mzima, weka dawa ya meno ijae eneo lote la brashi ya kwenye mswaki (1400-1500 ppmF-dawa ya meno ya watu wazima)," alisema.

Dk. Nzobo alisisitiza kwa kutoa wito kwa wananchi kwamba matumizi sahihi ya dawa ya meno na yenye kiwango cha ubora wa madini ya floridi na ujazo wa kila siku huundoa athari hasi kwa kinywa.

Alisema kiwango cha wagonjwa wanaopatiwa matibabu ya kinywa na meno nchini inakua huku akibainisha kuwa kuanzia Julai, mwaka jana, hadi Juni, mwaka huu, watu 535,324 waliohudhuria kwenye vituo vya kutolea matibabu nchini, walibainika kuoza meno.

Kati yao, alisema wagonjwa 219,482 sawa na asilimia 41, walifanyiwa matibabu ya kuziba jino (kutibu jino) kwa kuziba kwa dawa ya kudumu; kuziba kwa dawa ya muda na kutibu mzizi wa jino (root canal treatment).

Alisema lengo kuu la serikali kupitia Wizara ya Afya ni kuhakikisha inatibu meno ya watu kwa asilimia 60 na si kuyang'oa.

"Kabla ya uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali, miaka ya nyuma tulikuwa tunaziba kwa asilimia mbili na kung'oa watu meno kwa asilimia 98. Kwa sasa mambo yamebadilika na yatazidi kuwa bora zaidi mpaka lengo la kuziba kwa asilimia 60 litakapofikiwa ndani ya muda mfupi.

"Hospitali za rufani za mikoa zinazoziba meno watu wengi kuliko kung'oa ni 23 nchini ikiwamo Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya (MZRH). Zingine zenye hadhi ya rufani kimkoa ni Mawenzi, Mount Meru Njombe, Simiyu, Mwalimu Nyerere Memorial, Temeke, Songwe, Singida, Manyara, Iringa, Geita na Bukoba.

"Pia zimo Amana, Morogoro, Dodoma, Sekotoure, Sumbawanga, Tanga, Sokoine, Shinyanga, Maweni na Shinyanga," alisema.

Dk. Nzobo alizitaja pia hospitali 38 za wilaya nchini zinazoziba meno (kuyatibu) kwa wingi kuliko kuyang'oa ni Makambako, Arusha, Bagamoyo, Bariadi, Bukombe, Chato, Frelimo na Geita.

Zingine ni Hai, Handeni, Igunga, Ikungi, Kalambo, Karagwe, Kigamboni, Kiomboi, Kondoa, Korogwe, Kyela, Ulanga, Mbarali, Meru, Misungwi-Iteja, Monduli, Mtowisa, Muheza, Ngorongoro, Nsimbo, Nzega, Rombo, Rorya na Siha.

"Pia hospitali za Singida, Tanganyika, Tukuyu, Uvinza, Wanging'ombe na Vwawa inatibu maradhi hayo. Tanzania bila vibogoyo au watu wenye mapengo inawezekana," alisema.




Dk. Ronald Benju kutoka Maabara ya Vetinari Tanzania, akionyesha njia bora ya kutoa chanjo ya mbwa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kichaa cha Mbwa Duniani, wilayani Misungwi, mkoani Mwanza hivi karibuni. Kulia ni Ofisa Mwelimishaji na Ushauri Tiba Mwanza, Colman Edward. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHADEMA yakana kauli yenye utata ya BAZECHA

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimepinga kauli iliyotolewa na Baraza la Wazee wa chama hicho (BAZECHA) zenye viashiria vya udini na ukabila kikisema sio msimamo wao.

Juzi Mwenyekiti wa BAVECHA, Hashim Juma akizungumza katika hafla ya kusherehekea Siku ya Wazee Duniani alitoa kauli zinazoashiria udini na ukabila ikiwamo kumshangaa Rais Samia Suluhu Hassan kutosalimia kama dini inavyomtaka na badala yake anasalimia 'Jamhuri ya Muungano wa Tanzania'.

Aidha, alisema aliwasikia mashekhe wakilalamika kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, ana Makamu Mwenyekiti Bara, Tundu Lissu kuwa anamchukia Rais Samia Suluhu kwa sababu ya dini na eneo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, chama hicho hakihusiki na kauli zozote za kibaguzi zilizotolewa.

Alisema taarifa zilizotolewa zenye viashiria vya udini sio msimamo wa chama hicho na zinapaswa kupingwa na kila Mtanzania bila kujali dini, kabila, au mahali alipotoka.

Taarifa hiyo ilieleza pia mamlaka za chama hicho inafuatilia kiini cha kauli hizo na kuchukua hatua kwa mujibu wa Katiba, kanuni na miongozo ya chama.

RIPOTI MAALUM

# Gesi yageuka mateso kwa madereva magari na bajaji



Bajaji zinazotumia gesi, zikiwa kwenye foleni ya kujaza nishati hiyo, katika eneo la Uwanja wa Ndege, jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Na Halfani Chusi**

MOSHI wa magari yanayotumia mafuta unasababisha vifo vya watu 385,000 kila mwaka. Rai ya serikali ni wananchi waachane na matumizi ya mafuta, watumie gesi.

Lakini Tanzania hivi sasa ina vituo vitano tu vya kujaza gesi katika magari, vitatu vikiwa mkoani Dar es Salaam ambako madereva wa magari na bajaji wanakaa hadi saa nane kwenye foleni ya kujaza gesi, huku serikali ikikiri vituo vilivyoko vimeelemewa na wingi wa wahitaji.

Ni dosari changamoto iliyoibuka kipindi ambacho kuna mwitikio mkubwa wa wamiliki wa vyombo vya moto kutumia gesi ili kulinda mazingira.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe katika vituo vitatu vinavyotoa huduma hiyo mkoani Dar es Salaam; Ubungo, TAZARA na Uwanja wa Ndege, umebaini baadhi ya madereva wanapokwenda kituoni kujaza gesi, hukaa kwenye foleni zaidi ya saa nane hadi kupata huduma hiyo. Vituo vingine ni viwili vya kujaza gesi katika vyombo vya moto nchini, viko Mkuranga (Pwani) na Mtwara.

Thomas Samson dereva bajaji na mkazi wa Sinza, wilayani Kinondoni aliyekutwa kituo cha kujaza gesi Ubungo, anashauri huduma hiyo iwekwe katika kila kituo cha mafuta jijini.

"Kuna siku unakaa zaidi ya saa tano hadi nane kupata huduma kutokana na foleni. Sisi tunaofanya biashara ya usafirishaji, hali hii ni kupoteza muda wa kutafuta fedha. Kuna wakati unasema uje usiku wa manani, lakini napo pia unakutana na foleni," analalama.

Dereva huyo anasema baada ya kufunga mfumo wa gesi katika bajaji, gharama ya kujaza gesi ni Sh. 6,000 hadi Sh. 7,000, lakini anapata wastani wa kati ya Sh. 80,000 hadi Sh. 100,000 kutokana na matumizi ya gesi hiyo.

Dereva mwingine anayeegesha bajaji yake Magomeni, wilayani Kinondoni, Rashidi Bakari anasema:

"Katika vituo vya gesi vilivyoko Dar es Salaam vyenye uhakika ni cha Ubungo na Uwanja wa Ndege. Ukienda cha TAZARA wakati mwingine huduma hukosekana kwa sababu wao wanategemea gesi kutoka kituo cha Ubungo.

"Hakijaunganishwa na bomba la gesi kama kituo cha Ubungo lakini pia cha Uwanja wa Ndege angalau kina pampu sita za kujazia gesi, hivyo pale wanahudumia bajaji na magari mengi kwa wakati mmoja," anasema.

Martin Msafiri, mkazi wa Kigamboni, analalama kupoteza muda mwingi kwenye foleni ya kujaza gesi katika gari lake. Anataja adha hiyo ni kikwazo katika harakati zake za utafutaji (uchumi).

"Unakuta zaidi ya magari 100 yamekutangulia, unapoteza muda wote wa kuingia barabarani kutafuta ridhiki, inaumiza sana," anasema Msafiri.

Kiango Mgwale, aliyekutwa katika foleni kituo cha Uwanja wa Ndege, anasema alifika kituoni huko saa tano asubuhi, lakini hadi wakati huo (saa tisa alasiri) alikuwa hajapata huduma hiyo.

"Gesi ni rasilimali yetu wenyewe, lakini kuitumia ni tatizo. Serikali iangalie namna ya kuitawanya nchi nzima," anashauri.

Muuzaji wa gesi katika kituo cha Ubungo, Joe Chimazi, anakiri kituo kuelemewa na wateja kutokana na mwitikio mkubwa wa wananchi kwenye matumizi ya gesi, ukichangiwa na gharama zake kuwa ndogo kulinganisha na matumizi ya petroli na dizeli.

Anabainisha kuwa kwa siku wanahudumia zaidi ya bajaji na magari 1,000 yanayokwenda kupata huduma katika kituo hicho.

"Mfumo huu unawapa faida kubwa zaidi wenye magari makubwa, wanaweza kujaza gesi ya Sh. 100,000 wakaenda Iringa na kurudi na kwa kutumia mafuta, umbali huo ni zaidi ya Sh. 500,000," anasema.

Katika kituo cha TAZARA, Meneja Utawala Mary Aloyce, anataja changamoto kubwa ni kuishiwa gesi kunakotokana na idadi ya wahitaji wanaokwenda kupata huduma hiyo.

"Sababu kubwa ni kwamba, tunategemea gesi kutoka katika kituo cha Ubungo, hivyo wakati mwingine huwa tunaikosa na kusababisha wateja kusubiri kwa muda," anasema.

Mary anataja changamoto nyingine kituoni huko ni kuwapo bomba moja linalojaza gesi na kusababisha kushindwa kutoa huduma haraka kwa wateja.

Julai 29 mwaka huu, saa nane mchana, mwandishi wa habari wa Nipashe alizuru kituoni huko. Huduma ilikuwa imesitishwa, lakini aliona wateja waliosema walikuwa wanasubiri gesi iliyofuatwa kwa gari kituo cha Ubungo.

Mwandishi pia alitembelea kituo cha Uwanja wa Ndege ambako Msimamizi wa Shughuli na Matengenezo, Levocatus Lameck, aliungana na wenzake wa TAZARA na Ubungo kwamba wameelemewa wateja kiasi cha kuwa na foleni ndefu za magari na bajaji vituoni.

"Bei ya gesi ni nusu ya ile ya mafuta. Kwa mfano, mtu anayetumia gari aina ya Toyota IST, Raum, Vits, akifunga mtungi wa gesi wa kilo 11, anaujaza kwa Sh. 17,000 na akatembea umbali wa kilometa 180 huku amewasha kiyoyozi.

"Hapa tunaongelea umbali wa kutoka Dar es Salaam kwenda Morogoro ambapo kwa mafuta mtu huyo angetumia zaidi ya Sh. 120,000.

"Kwa bajaji mtu ambaye ana mtungi wa kilo nne na nusu, anatumia Sh. 6,800 kujaza, anaweza kutembea umbali wa Km 240. Unaweza kuona mtu kama huyo ni kwa namna gani anaokoa fedha nyingi, ni mara mbili ya kiwango ambacho angeweza kutoa," anafafanua.

Lameck anasema kwa takwimu ambazo si rasmi, kuna zaidi ya bajaji 3,500 zenye mfumo wa gesi ambazo kwa siku wao huhudumia zaidi ya bajaji 600 na magari zaidi ya 1,000.

Anasema kuwa kituo hicho kina pampu sita zinazohudumia magari sita kwa dakika nne hadi tano. "Tuna mikonga ya kujazia gesi sita, hivyo kwa mara moja tunajaza katika vyombo sita na presha yake ni kubwa. Ninashauri kama vikijengwa vituo vingine, viige mfumo wetu huu," Lameck anasema.

**HATUA SERIKALINI**

Kaimu Mkurugenzi wa Biashara ya Gesi na Mafuta wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Emmanuel Gilbert, anakiri vituo vya kujaza gesi mkoani Dar es Salaam kuelemewa na wingi wa wahitaji wa nishati hiyo.

Anasema msongamano mkubwa unaoshuhudiwa hivi sasa vituoni umetokana na kuongezeka kwa uelewa wa matumizi ya gesi asilia na gharama ndogo kulinganisha na matumizi ya mafuta.

Anasema kuwa awali wananchi walikuwa wanasita kutoka na ugeni wa teknolojia, akiwa na ufafanuzi kuwa, "teknolojia ikiwa mpya, watu wengi huwa wanakuwa na wasiwasi kidogo, nini kinaweza kutokea, pia usalama upoje."

Gilbert anasema tayari serikali imeona tatizo na imeshaanza kuchukua hatua na matokeo yameanza kuonekana.

"Kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015, gesi ilikuwa ni haki ya TPDC pekee, lakini serikali ikaona TPDC peke yake haina uwezo wa kusambaza huduma hiyo nchi nzima kutokana na mwamko wa watu na uhitaji kuwa mkubwa kutumia gesi asilia katika magari yao na bajaji.

"Kutokana na hali hiyo, tuliamua kutanua wigo kwa kuita wawekezaji binafsi na tayari kwa sasa wapo ambao wameshaanza kuwekeza," alisema.

Katika hilo, Gilbert anasema kituo cha Uwanja wa Ndege kilichozinduliwa Desemba mwaka jana, ni cha kampuni binafsi na kinafanya vizuri na ndicho tegemeo zaidi hivi sasa kutokana na uwezo wake wa kujaza magari sita kwa wakati mmoja.

"Sasa kampuni hiyo hiyo ina mpango wa kujenga kituo kingine barabara ya Sam Nujoma, halafu sisi TPDC tunajenga kituo kikubwa maeneo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) jirani na Hosteli za Dk. John Magufuli kitakachowezesha kutoa gesi kutawanya katika vituo vingine," anasema.

Anakitaja ni kituo hicho ambacho kitaleta ushindani katika soko kwa kuwa kitakuwa na uwezo wa kusambaza gesi kwa vituo vidogo ambavyo havijaunganishwa na miundombinu ya gesi asilia.

"Isivyo bahati, kituo cha Ubungo kimefikia mwisho, hakina uwezo wa kutoa gesi kwenda kwenye vituo vinavyotarajiwa kujengwa, hivyo huduma hiyo itaanza kupatikana Desemba mwaka huu tutakapomaliza ujenzi wa kituo cha TPDC na kitakuwa na uwezo mkubwa kuliko cha Ubungo.

"Pia tuna uhakika gesi inaweza kutoka pale ikafika Morogoro, Tanga na Dodoma na katika mikoa mingine itategemeana na wawekezaji watakavyochangamkia fursa," anasema Gilbert.

***ITAENDELEA KESHO**

**HABARI KITAIFA**

# Mchungaji kuchunguzwa madai kuendesha maombi chonganishi

**Na Alex Sayi,** MASWA

SERIKALI mkoani Simiyu imeanza uchunguzi dhidi ya huduma zinazotolewa na Mchungaji wa Kanisa la International Evangelical Assembles of God Tanzania (IEAGT) kwa madai ya kufanya maombezi chonganishi.

Uchunguzi huo umeanza kutokana na agizo lililotolewa juzi na Mkuu wa Mkoa, Kenani Kihongosi, kwa Mkuu wa Wilaya ya Maswa wakati akizungumza na wakazi wa kata ya Shishiyu katika ziara yake ya kikazi iliyolenga kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Kigonhosi alisema maombezi yanayofanywa katika kanisa hilo ni chonganishi kutokana na watu kutajwa majina wakati wa maombi kuwa ni wachawi kwa madai kuwa mapepo yamepanda.

"Mkuu wa wilaya hili suala liko chini yako na fuatilia uhalali wa kanisa hili. Haiwezekani mchungaji aendeshe ibada zinazotaja majina ya watu na kuwatuhumu kuwa ni wachawi kisa mapepo yamepanda. Hizi ni ramli chonganishi kama zingine," aliagiza.

Kihongosi alimtaka mchungaji huyo kuhakikisha mapepo hayo hayataji tena majina ya wakazi wa eneo hilo kwa kuwa ibada hiyo inaleta taharuki kwa wananchi na kuwafanya waishi maisha ya hofu.

"Wewe kama ni mtaalamu wa kuzungumza na mapepo, sasa yaambie hayo mapepo yaache kutaja majina ya watu na kuwatuhumu kuwa ni wachawi na unajua serikali ina uwezo wa kufungia kanisa lolote linalohatarisha usalama wa wananchi," alisema Kihongosi.

Akitoa utetezi katika mkutano huo, Mchungaji wa Kanisa hilo, Joseph Jackson, alisema hajamtuhumu mtu yeyote kuwa ni mchawi isipokuwa ni waumini wanaofika kanisani hapo kufanyiwa maombi na kuwa mapepo yakipanda, wanaanza kutaja majina ya wachawi hao.

"Mkuu wa Mkoa mimi sijawahi kumtaja mtu yeyote kuwa ni mchawi. Wanaonituhumu waseme vizuri. Mimi natoa huduma ya kuombea watu walio na mapepo nikiyauliza yametoka wapi ndipo huwa yanawataja," alisema.

Awali, akitoa malalamiko kwa mkuu huyo wa mkoa, mmoja wa waathirika wa maombezi ya mchungaji huyo, Pili Kidesela, mkazi wa kata ya Shishiyu, alisema mchungaji huyo amekuwa kero kwa wakazi wa eneo hilo kwa kuendesha ibada zinazowatuhumu wakazi hao kuwa wachawi.

"Nimetuhumiwa kuwa ni mchawi na si mimi peke yangu bali wakazi wengine hapa Shishiyu wametuhumiwa uchawi. Hii hali inatufanya tuishi kwa hofu katika eneo letu kutokana na huduma yake huyu mchungaji," alisema Kidesela.

Mkazi mwingine, Lucia Marko, alisema katika maombezi ya mchungazi huyo amewahi kutajwa kuwa mmoja wa wachawi wanaowaloga waumini wa kanisa hilo.

"Mimi nilishatuhumiwa kuwa huwa naenda kanisani hapo kuwaloga waumini wa kanisa hilo. Nilituhumiwa hivyo baada ya muumini wa kanisa hilo kupandisha mapepo na kunitaja kuwa aliniona," alisema.

Naye Marko Mashauri alisema mchungaji huyo amekuwa akiendesha ibada hizo chonganishi kwa kutaja majina ya wanawake kijijini hapo na kuwatuhumu kuwa wachawi.

Nipashe ilimtafuta mtendaji wa kata hiyo ili kujua kama amewahi kupokea malalamiko ya namna hiyo na alikiri kuyapokea na kuwa alishawahi kumwita na kumtaka aachane na mafundisho hayo lakini hakuwa tayari kufanya hivyo.

Alisema baada ya hapo, ilibidi atoe taarifa kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Aswege Kaminyoge, aliyeahidi kulifanyia kazi ili kudhibiti taharuki iliyozuka kwa wananchi wake. Naye Kaminyoge alisema licha ya uchunguzi juu ya maombezi ya mchungaji huyo, amewahi kukutana naye awali na kumuzia masuala hayo lakini hakuwa tayari kutii agizo hilo.

# Tanzania yaanika utajiri nishati jotoardhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMPUNI ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) imesema imeainisha maeneo 52 katika mikoa 16 yenye uwezo wa kuwa na nishati jotoardhi.

Meneja Mkuu wa TGDC, Mathew Mwangomba, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano la 10 la Jotoardhi Afrika litakalofanyika Oktoba 21 hadi 27, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Alisema Tanzania ina uwezo wa kupata zaidi ya megawati 5,000 za nishati ya umeme na nishati ya joto megawati 15,000 kwa ajili ya matumizi ya moja kwa moja.

"Kampuni hii inaendelea na miradi yake mitano ya kipaumbele ambayo inalenga kuzalisha megawati 200 za umeme. Miradi hiyo ni Ngozi 70MW (Mbeya), Kiejo-Mbaka 60MW (Mbeya), Natron 60MW (Arusha), Songwe 5MW, na Luhoi 38MW (Pwani) na kufanya jumla ya megawati 200," alisema.

Alisema serikali imewawezesha kununua mtambo wa kuchoronga visima vya utafiti vya jotoardhi wenye thamani Sh. bilioni 13.18 na utatumika katika mradi wa ngozi na miradi mingine ya jotoardhi nchini.

"Uchorongaji wa visima vya utafiti katika mradi wa ngozi unatarajia kuanza muda mfupi kutoka sasa baada ya kukamilika kwa taratibu za ununuzi," alisema.

Alibainisha kuwa kupitia miradi hiyo, Tanzania inalenga kupunguza utegemezi nishati ya mafuta, gesi na maji kuimarisha usambazaji wake wa umeme.

Kuhusu kongamano hilo, Mwangomba alisema litasaidia upigaji wa hatua katika kukamilisha safari ya jotoardhi duniani.

Alisema katika kongamano hilo watu 1000 kutoka nchi zikiwamo za Afrika na mataifa mengine ya ulaya na uarabuni 13 wanatarajia kushiriki.

"Kongamano hili limepangwa kufunguliwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango Oktoba 23 mwaka huu na kufungwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Oktoba 25, mwaka huu," alisema.

Alitaja mada zitakazojadiliwa katika kongamano hilo ni uzalishaji wa umeme kwa kutumia jotoardhi, matumizi ya moja kwa moja ya jotoardhi katika sekta kama kilimo na ufugaji hasa wa samaki, uhandisi wa visima vya jotoardhi na teknolojia mpya, njia za kupata ufadhili wa miradi ya nishati mbadala ikiwamo nishati ya jotoardhi.


Canara Bank (Tanzania) Ltd.

(Together we can build a better life)

**PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES**

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER**

| S/N | DESCRIPTION | | FEES AND CHARGES TZS | USD |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Monthly Maintanance** | SA | 2,000.00 | 2 |
| | | CA | 6,000.00 | 4 |
| 2 | **Non Maintanance of Minimum Balance** | SA | 1,500.00 | 2 |
| | | CA | 4,000.00 | 4 |
| 3 | **Account Statement Charges** | SA-Monthly | - | 0 |
| | | SA-Interim | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| | | CA-Monthly | Free | Free |
| | | CA-Interim | 1,500.00 per page | 1.5 per page |
| 4 | **Cash withdrawal** | SA-Up 25M | Free | |
| | | SA-Over 25M | 0.26% | |
| | | SA-Up to $2K | | Free |
| | | SA-$2K-$5K | | 0.60% |
| | | SA-Over $5k | | 0.60% |
| | | CA-Up to 25 M | Free | |
| | | CA-Above 25M | 0.26% | |
| | | CA-Up to USD 5K | | Free |
| | | CA-$ 5K-$10K | | 0.60% |
| | | CA-Above $ 10K | | 0.60% |
| 5 | **Cash Deposit Charges** | SA-Up to 25M | Free | |
| | | SA-Over 25M | 0.22% | |
| | | SA-Up $5K | | Free |
| | | SA-Over $5K | | 0.50% |
| | | SA-small currency ($1 to $20) | | 10.00% Minimum charge $1 |
| | | CA-Up to 50M | Free | |
| | | CA-Over 50M | 0.22% | |
| | | CA-Up to $10K | | Free |
| | | CA-Over $10K | | 0.50% |
| | | CA-small currency ($1 to $20) | | 10.00% Minimum charge $1 |
| 6 | **Balance Confirmation Certificate** | SA | 12,800.00 | 10 |
| | | CA | 21,200.00 | 13 |
| 7 | **Account Closure Charges** | SA | 20,000.00 | 20 |
| | | CA | 50,000.00 | 50 |
| 8 | **Activation of Dormant Account** | SA | Free | Free |
| | | CA | Free | Free |
| 9 | **Stop Payment Charges** | SA | Free | Free |
| | | CA | 35,000.00 | 28 |
| 10 | **Cheque Return Charges/Dishonoured Cheque** | CA-Inward | 50,000.00 | 50 |
| | | CA-Outward | 50,000.00 | 50 |
| 11 | **Cheque Clearing Charges** | CA-Inward | 1,300.00 | 1 |
| | | CA-Outward | Free | Free |
| 12 | **Ledger folio charges per folio (40lines per** | SA | Free | Free |
| | | CA | 6,000.00 | 4.00 |
| 13 | **Cheque book Charges** | CA-50 Leaves | 42,000.00 | 27 |
| 14 | **Mobile Banking** | | | |
| i | Withdrawal Charge | Upto 100,000 | 1,700.00 | N/A |
| | | 101,000 to 200,000 | 2,600.00 | N/A |
| | | 201,000 to 400,000 | 4,300.00 | N/A |
| | | 401,000 to 600,000 | 5,100.00 | N/A |
| | | 601,000 to 999,000 | 6,800.00 | N/A |
| ii | Funds Transfer/Mobile Wallet | Upto 100,000 | 500.00 | N/A |
| | | 101,000 to 250,000 | 900.00 | N/A |
| | | 251,000 to 500,000 | 1,700.00 | N/A |
| | | 501,000 to 1,000,000 | 4,300.00 | N/A |
| | | 1,001,000 TO 10 Mn | 8,500.00 | N/A |
| 15 | **Locker Rent-Yearly** | Small | 296,700.00 | N/A |
| | | Medium | 508,500.00 | N/A |
| | | Big | 635,600.00 | N/A |
| 16 | **Remittances** | | | |
| i | TISS | Any amount per 1 | TZS 8,450.00 | TZS 8,450.00 Equivallent |
| ii | E Remittances | Upto USD 1000 or Eq. TZS | 17,000.00 | $ 9.00 |
| | | 1001 to 5000 | 20,400.00 | $ 11.00 |
| | | 5001 to 10000 | 40,700.00 | $ 22.00 |
| | | 10,001 and above | 84,800.00 | $ 43.00 |
| iii | Swift Outward | Upto 5,000 | NA | $ 39.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 51.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 77.00 |
| iv | Swift Inward | Upto 5,000 | NA | $ 11.00 |
| | | 5,001 to 10,000 | NA | $ 16.00 |
| | | above 10,000 | NA | $ 26.00 |

| | |
|---|---|
| HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | 02-OCT-24 |
| GM-CREDIT | 02-OCT-24 |
| HEAD BUSINESS OPERATIONS | 02-OCT-24 |

| S/N | DESCRIPTION | | FEES AND CHARGES TZS | USD |
|---|---|---|---|---|
| 17 | **Loan/Advances Related Charges** | | | |
| i | Processing Charges | Upto 5 Mio - | 21,200.00 | |
| | | 5Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | |
| | | 10 Mio to 25mio - | 339,000.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | |
| | | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | |
| | | Upto 5,000 - | | $85.00 |
| | | 5000 to 10,000 - | | $170.00 |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.28% |
| | | >500,000--* | | 1.06% |
| ii | Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | |
| | | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | |
| | | Upto 50,000 | | FREE |
| | | >50,000 - (Min 150) | | 0.26% |
| iii | Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - | 21,200.00 | |
| | | 5 Mio to 10 Mio - | 169,500.00 | |
| | | 10Mio 25mio - | 381,400.00 | |
| | | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | |
| | | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | |
| | | Upto 20,000 - | | $255.00 |
| | | 20,000 to 500,000 - | | 1.53% |
| | | >500,000--* (*minimum 9000) | | 1.28% |
| iv | Inspection Charges | Upto 100 Mio - | 21,200.00 | |
| | | >100 mio - | 42,400.00 | |
| | | Upto 50,000 | | $22.00 |
| | | >50,000 | | $43.00 |
| v | Credit Reference Report Charges | | 101,700.00 | $43.00 |
| vi | Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other bank/lenders | 2.00% | 2.00% |
| 18 | **Guarantees (Local & International)** | | | |
| i | Bonds & Guarantees | per quarter (Min TZS 75,000) | 1.02% | 1.02% |
| ii | Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | 0.43% |
| 19 | **Letter of Credit** | | | |
| 19.1 | **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | |
| i | Opening commission | commission Min $ 200 | NA | |
| ii | LC amendment Commission | Commision Min $50 max 350 | NA | 1.02% |
| iii | Swift charge for LC opening | | NA | 0.34% |
| iv | Swift charge for other message/amendments | | NA | $34.00 |
| v | Extensions - Commissions | commission Min $ 200 | NA | $34.00 |
| vi | LC cancellation charges | commission Min $ 200 | NA | 1.02% |
| vii | Non payment of Bills on due date | Till Payment | NA | 1.02% |
| 19.2 | **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | |
| i | Advising commission | | NA | $119.00 |
| ii | Confirmation Commission | Commision Min $150 | NA | 0.43% |
| iii | Negotiating bills under LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% |
| iv | Reimbursement claim paid | Commision Min $75 | NA | 0.43% |
| v | Extensions - | Commision Min $200 | NA | 1.02% |
| vi | Collection of Export LC | Commision Min $75+cuourier+interest | NA | 0.43% |
| vii | Amendments | | NA | $64.00 |
| 20 | **Other disclosures** | | | |
| i | Base or Prime Lending Rate | | 16% | 10% |
| ii | Maximum spread | | 5% | 5% |
| iii | Penal Interest | | | |
| | a.For non compliance on Terms of Saction | Rate per year over regular rate of interest | 3% | 3% |
| | b.For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | Rate per year over regular rate of interest | 5% | 5% |
| vi | Deposit Rates | | | |
| | a. Current account | | Nill | Nill |
| | b. Savings bank deposit | | 3.00% | 1.00% |
| | C. Fixed Deposits Rates | **Up to TZS 50 M(up to USD 50,000)** | | |
| | | 30 -90days | 3.50% | 1.50% |
| | | 91-180days | 4.50% | 2.25% |
| | | 181-364 days | 5.50% | 3.00% |
| | | 1 year and above | 8.00% | 3.75% |
| | | 2 Years and Above | 8.00% | 4.00% |
| | | **TZS 50 M-100M (USD 50,000 -USD 100,000)** | | |
| | | 30 -90days | 4.50% | 2.25% |
| | | 91-180days | 5.50% | 2.50% |
| | | 181-364 days | 7.00% | 3.50% |
| | | 1 year and above | 8.25% | 4.25% |
| | | 2 Years and Above | 9.00% | 4.75% |
| | | **Above 100 M(Above USD 100,000)** | | |
| | | 30 -90days | 5.50% | 2.50% |
| | | 91-180days | 6.50% | 3.25% |
| | | 181-364 days | 7.50% | 4.00% |
| | | 1 year and above | 8.50% | 4.75% |
| | | 2 Years and Above | 9.50% | 5.00% |



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Ally Senga (kushoto), akikata utepe kuzindua magari 11 ya Jeshi la Magereza, yaliyonunuliwa kwa fedha za bajeti za mwaka wa fedha 2023/2024, kwa ajili ya kutoa huduma katika magereza mbalimbali nchini. Wengine ni Kamishna Jenerali wa Magereza, Jeremiah Katungu (wa pili kulia), na (kulia) ni Kamishna wa Sheria na Uendeshaji wa Jeshi hilo, CP Nicodemas Tenga. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Wanasheria wa UK, 'Sauzi' kumsaidia Kabendera rufani dhidi ya Vodacom

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya Mahakama Kuu kutupa shauri la madai lililofunguliwa na mwanahabari Erick Kabendera dhidi ya kampuni ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania, wanasheria kutoka Afrika Kusini na Uingereza wanatarajia kumsaidia kukata rufani kupinga uamuzi huo.

Mahakama Kuu Masjala Ndogo ya Dar es Saalam mwezi uliopita ilitupa shauri la mwanahabari huyo kudai kampuni hiyo kumlipa Sh. bilioni 28 kwa madai ilifanikisha kutekwa kwake, ikiunga mkono hoja kwamba halikuwa mahakamani kihalali.

Katika tamko lake kwa waandishi wa habari jana, Kabendera alieleza hatua inayofuata baada ya Mahakama Kuu kuifuta kesi ya madai (12799/2024) aliyofungua dhidi ya Vodacom Tanzania Ltd mwezi Julai 2024.

Kabendera alisema kuwa Juni 29, 2019, akiwa nyumbani kwake, Mbweni Mpiji, Dar es Salaam, alivamiwa na watu wasiojulikana na kuzingira nyumba yake. Baada ya purukushani wakajitambulisha kuwa ni askari kutoka vyombo tofauti vya dola ambao walikwenda kumkamata kwa makosa ambayo hayakujulikana wakati huo.

Hata hivyo, alidaiwa kuwa akiwa mikononi mwao huku amefungwa pingu mkononi ndani ya gari yao, walimwambia maneno "Wewe ni mjinga, umekataa kuunga mkono juhudi na sasa utakiona cha mtema kuni."

"Taarifa za kutafutwa kwangu na kuwa maisha yangu yalikuwa hatarini, zilianza kusambaa Mei mwaka 2019. Tuhuma kubwa dhidi yangu ilikuwa ni kuikosoa serikali ya Rais Magufuli kupitia kazi yangu ya uandishi.

"Jambo la kushangaza ni kwamba nilikuwa ninafuatwa kila sehemu niliyokuwa ninakwenda na watu wasiojulikana katika kipindi hiki chote. Nilianza kupata hofu kubwa pale nilipokuwa na mwandishi mwenzangu katika gari saa saba usiku tarehe 20 Mei 2024 tukitoka kumsalimia rafiki yetu aliyekuwa mgonjwa, tulipokoswakoswa kupigwa risasi na kikundi cha watu mwenye magari manne eneo la Bahari Beach. Tulitoa ripoti ya tukio hilo kwenye Kituo cha Polisi Kunduchi.

"Wasiwasi uliendelea kuwa mkubwa baada ya kuwasha simu tarehe 29 mwezi Juni 2019 saa tisa alasiri na kugundua kuwa haikuwa na mawasiliano. Nilifanya hivyo ili kuweza kuchukua fedha kutoka kwenye namba yangu ya simu (+255767456796) ili niweze kumnunulia dawa mama yangu aliyekuwa mgonjwa.

"Niliamua kuwapigia huduma kwa mteja ya kampuni ya Vodacom kuuliza sababu zilizopelekea simu yangu kuzimwa bila taarifa. Hata hivyo, wahudumu wa Huduma kwa Wateja walinielekeza niende kwenye Ofisi za Vodacom zilizoko jengo la Kibo Complex, eneo la Tegeta kwa msaada zaidi.

"Baada ya kuhoji ulazima wa kufanya hivyo, nilifahamishwa kuwa laini yangu ilikuwa na tatizo la kiufundi ambalo nilihitajika kwenda kwenye ofisi zao ili waweze kulitatua.

Kauli hiyo ilinipa wasiwasi kutokana na ukweli kwamba nilikuwa ninawafahamu watu zaidi ya wanne waliokuwa wamepewa maelekezo kama yangu na kampuni za simu nilitoa taarifa kwa watu, vyombo vya usalama waliofika na kuwachukua watu bila hata makosa yao kujulikana. Ushirikiano usiokuwa wa kawaida kati ya vyombo vya usalama na kampuni za simu ulinipa wasiwasi kiasi kwamba nilihisi kuwa nilikuwa nimewekewa mtego," alidai.

Aliendelea kudai, kama ilivyokuwa Mahakama Kuu Masjala Ndogo ya Dar es Salaam, "Kampuni ya Vodacom ilihusika moja kwa moja katika kufanikisha utekaji wangu.

Pili, bila watumiaji mitandao ya kijamii, vyombo vya habari kusambaza taarifa kwa kasi, ni wazi kwamba ningeweza kupotezwa na pengine kuuawa.

"Kabla ya kusikilizwa kwa ushahidi huo kwenye mahakama ya Tanzania, kesi yangu iliwekewa pingamizi na kushindwa kuendelea. Baada ya kushauriana na jopo la wanasheria, tumekubaliana yafuatayo:

"Kwanza, kukata rufani kwenye Mahakama ya Rufani dhidi ya pingamizi lililowekwa dhidi yetu kwa kuwa tunaamini kuwa kesi yetu ina mashiko na inastahili kusikilizwa ili tuweze kuwakilisha ushahidi wetu mbele ya mahakama ambapo tunaamini una nguvu za kuhakikisha tunatendewa haki.

"Kutokana na ushahidi tuliokusanya baada ya miaka mitatu ya uchunguzi, tumeona kuwa ushahidi ni mkubwa kiasi kwamba unatosha kuishitaki Vodacom Tanzania na kampuni zake tanzu nchini Afrika ya Kusini na Uingereza. Wanasheria wangu kutoka Uingereza na Afrika ya Kusini wanakamilisha utaratibu wa kufungua kesi dhidi ya Vodacom Group South Africa na Vodafone Group PLC ambayo ina makao yake makuu Uingereza haraka iwezekanavyo," alisema Kabendera.

# Sungusungu wanaojifanya mahakama kukiona

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amesema hayuko tayari kuwavumilia askari wa jeshi la jadi, maarufu sungusungu, wanaojifanya mahakama na kutoa hukumu mbalimbali kwa wananchi wanaodaiwa kutenda makosa bila kufuata utaratibu wa kisheria.

Macha alitoa onyo hilo juzi wakati akizungumza na askari wa jeshi hilo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Manyada wilayani Shinyanga mkoani hapa.

Alisema sungusungu wamekuwa na tabia ya kutoa adhabu kwa wananchi zikiambatana na kuwatenga kujihusisha na chochote ndani ya jamii pale wanapowakuta wana makosa.

Macha alikemea vitendo hivyo na kusema kwa mujibu wa sheria za nchi, jukumu la kutoa hukumu ni la mahakama pekee na si mtu yeyote, hivyo kuwataka kuzingatia sheria za nchi.

Alisema serikali inatambua mchango wa jeshi hilo katika kuhakikisha amani na utulivu vinaendelea kutawala ndani ya jamii kwa kudhibiti vitendo vya kihalifu, hivyo kulitaka linapokuwa kwenye utekelezaji wa majukumu yake, askari wazingatie sheria nchi badala ya kujichukulia sheria mkononi na kutoa adhabu kali kwa wahalifu na kuwatenga wananchi.

Mkuu huyo wa mkoa pia aliwataka sungusungu kushiriki kikamilifu kuzuia tatizo la mmomonyoko wa maadili kwa vijana kuanza ngazi ya vitongoji kwa sababu limeonekana kuwa janga kubwa katika taifa.

Kamanda wa Sungusungu Mkoa wa Shinyanga, John Kadama, alisema wako tayari kufuata sheria za nchi na kwamba watashirikiana vyema na serikali katika kulinda usalama wa raia na mali zao.


HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

TANGAZO LA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KITALU "DA" NA "N"

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA ANAWATANGAZIA WANANCHI WOTE AMBAO HAWAJAKAMILISHA MALIPO YA UNUNUZI WA VIWANJA KATIKA MRADI WA VIWANJA ENEO LA KIKOMBO KATIKA KITALU "DA" NA "N" KUWA WANATAKIWA KUKAMILISHA MALIPO YOTE NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14) KUANZIA TAREHE 3 HADI 16 OKTOBA, 2024.

KUSHINDWA KUKAMILISHA MALIPO HAYO; KIWANJA HICHO KITATOLEWA KWA MWOMBAJI MWINGINE BILA TAARIFA ZAIDI KWAKO NA WEWE UTAREJESHEWA FEDHA YAKO BAADA YA KUKATWA ASILIMIA 10 KWA GHARAMA ZA USUMBUFU.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA MKURUGENZI WA JIJI LA DODOMA

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# DAWASA iseme kweli kuhusu upungufu huduma ya maji Dar

**KWA** takriban mwezi sasa, wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo ya jirani hususan Kibaha, wanapata shida ya maji hatua inayowafanya wapate adha kubwa ya kusaka huduma hiyo huku wengine wakitumia maji yasiyo salama kwa afya zao ambayo yanauzwa kwenye madumu na hayajulikani yanakotoka wapi.

Katika maeneo mbalimbali kama vile Tabata Segerea, Ubungo, Sinza, Kijitonyama, Saranga, Malamba Mawili, Kinyerezi, Kimanga na Kisukulu, ni jambo la kawaida kukutana na watu wakiwa wamebeba ndoo kichwani na wengine wakiwa na madumu kwenye mikokoteni. Yote hiyo inaonesha kuwa kuna tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

Pamoja na kwamba tatizo hilo limekuwa kubwa hivi sasa, wananchi katika baadhi ya maeneo wamebainisha kwamba tatizo hilo liko kwa zaidi ya mwezi sasa na limesababisha watumie muda mwingi kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za uzalishaji. Wako wengine ambao wamesema wanalazimika kuamka saa 11:00 alfajiri Kwenda kutafuta maji katika visima au kuvizia kama yanaweza kutoka hali ambayo inawaweka katika mazingira ya hatari ya kufanyiwa ukatili.

Katika eneo la Saranga wilayani Ubungo, kwa mfano, wananchi wamelalamika kuwa tatizo hilo kwa sasa ni sugu kwa kuwa wamekosa huduma hiyo kwa zaidi ya mwezi na wanapouliza Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA), hakuna majibu sahihi yanayotolewa zaidi ya kusema wavute subira huduma itarejea wakati wowote. Wakati maofisa wa DAWASA wakijibu hivyo, wananchi wanakumbwa na mshangao kwa sababu kuna wakati maji hayapatikani lakini mabomba barabarani yanatoa maji kutokana na kuwa yameharibika.

Eneo la Segerea ni mojawapo ya sehemu zilizokumbwa na tatizo hilo, huku kama ilivyo kwa wananchi wa Saranga, majibu yanayotolewa na watendaji wa mamlaka hayo si ya kutia matumaini ya kupata huduma hiyo. Wananchi hao wamekuwa wakisaka maji kutoka sehemu moja kwenda nyingine huku wakitegemea kununua maji kutoka kwa wauzaji kwenye madumu au visima vya watu binafsi.

Hali hiyo ya kukosekana kwa maji inakwenda kinyume cha matumaini yaliyokuwa yakitolewa na watendaji wa DAWASA waliyokuwa wakiyatoa hivi karibuni kwamba wameongeza kasi ya usambazaji wa huduma kwa wananchi huku wakijinasibu kuwa wananchi hadi wa pembezoni kama vile Mabwepande, Mpigi Magohe na Mbezi Msakuzi tayari wamefikiwa na huduma hiyo.

Kama kasi ya usambazaji wa huduma hiyo imeongezeka kutokana na uwekezaji wa mabilioni ya shilingi katika miradi ya maji mkoani Dar es Salaam na maeneo ya Pwani ni kubwa, iweje sasa wananchi wahangaike kupata huduma hiyo na kuyatafuta kwa tochi?


Kwa namna ilivyo sasa, kuna shida mahali ambayo pengine ni kubwa na haisemwi hadharani. Mazingira yanaonesha hivyo kwa sababu Juni 30, mwaka huu, Waziri wa Maji Aweso alifanya ziara katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Dar es Salaam, katika ziara hiyo, alishuhudia madudu yaliyosababisha aliyekuwa Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Kiula Kingu, na aliyekuwa Mkurugenzi wa Uzalishaji na Usambazaji Maji wa mamlaka hiyo, Shaaban Makwenywa, kusimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi wa tuhuma dhidi yao.

Wakati wa ziara hiyo, Aweso alitembelea Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), Mbezi, Mshikamano na Tegeta A alikoshuhudia matangi ya maji yakiwa hayana maji, hivyo kusababisha wananchi kutokupata huduma hiyo bila sababu zozote za msingi.

Katika mtazamo chanya, liko tatizo ndani ya DAWASA ambalo lazima linatokana na utendaji wa wafanyakazi na uongozi mbovu au tatizo la kifedha linaloikumba kiasi cha kushindwa kutimiza azma yake ya kuwapatia wananchi huduma ya maji ya uhakika. Lakini kama ni ukosefu wa fedha, mbona wananchi wanalipa tena wale wasiotimiza hilo wanakatiwa maji.

Ni vyema serikali kupitia Wizara ya Maji, yenye dhamana ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo mijini na vijijini, ikichukua hatua madhubuti kabla mambo hayajawa mabaya zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kamati shule, wazazi mlikabili la watoto kuzurura muda wa shuleni

Na Mwandishi Wetu

**KILA** mara wazazi na walezi wamekuwa wakitupiwa lawama kuwa ni chanzo cha watoto wao kukithiri kwa utoro shuleni, watoto wa mitaani na kujihusisha na vitendo viovu kwa kujiunga katika makundi yasiyofaa.

Migogoro ndani ya ndoa, nayo imekuwa ikielezwa kuchangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la watoto wengi wa mitaani, kukosa mwelekeo kwa kuwa na tabia mbaya na kupata malezi mabaya.

Hayo yote inawezekana kuwa yapo, isipokuwa ni zipo njia za kuhakikisha kwamba hayaendelei kutokea katika jamii kwa kuziba viashiria vyake.

Mbaya zaidi na jambo la kusikitisha, ni kitendo cha baadhi ya wanafunzi kuonekana wakizagaa mitaani na kwenye maeneo yasiyofaa kwa ajili ya ustawi wa makuzi yao.

Hapo ndipo baadhi ya watu waliposikika wakilalamikia baadhi ya shule kuwa zinachangia wanafunzi kukithiri kwa utoro kutokana na kurudishwa nyumbani bila ya wazazi na walezi wao kupewa taarifa kwa njia ya barua na simu.

Tangu shule zilipofunguliwa siku chache zilizopita, wanafunzi wengi wameshuhudiwa wakizagaa mitaani wakizurura huku na kule bila ya kuwa na sababu za msingi.

Wanafunzi wengine wameonekana maeneo ya sokoni 'wakichakura' mabaki ya bidhaa zilizotupwa, wengine wakiwinda ndege kwenye miti kwa kutumia manati na wengine mtoni na mabwawa wakivua samaki.

Wapo waliokutwa wakicheza mpira kwenye maeneo yaliyowazi na majumba makuu ambayo ujenzi wake haujamilika.

Wengine walikuwa wakicheza mchezo wa bao, kamari na mingine katika vichaka.

Mbaya zaidi, wako waliokutwa maeneo kunakoendeshwa biashara za vileo kwenye makazi ya watu, wakipambana kucheza kamali kwenye mashine maarufu kama bonanza. Mchezo huo uliokolea kwelikweli kutokana na wanafunzi hao kugawanyika katika timu mbili.

Kila upande ulikuwa ukishangilia mmoja unapoliwa na mwingine unapokula fedha ambazo zilipatikana kwa wao kuchangishana.

Kitendo hicho kiliwafanya hata wapiti njia katika sehemu hizo za biashara, kusimama ili kufahamu kulikoni, huku wengine wakipigwa na butwaa kutokana na vitendo hivyo kufanyika wakati wanafunzi hao wakitakiwa kuwa shuleni kwa kuwa ni muda wa masomo. Wanafunzi hao walipoulizwa kulikoni, wakasema wameamriwa na walimu kurudi nyumbani kwa wazazi na walezi wao kwenda kuchukua fedha kwa ajili ya kuchangia chakula cha mchana shuleni.

Ni kweli makuzi ya mtoto na malezi bora huanzia kwa mzazi na mlezi nyumbani, na anapokabidhiwa shuleni, inakuwa ni jukumu la mwalimu kuhakikisha anapata elimu bora.

Chakula cha mchana shuleni kwa mwanafunzi ni muhimu kwa sababu kinasaidia kumjenga katika afya bora, akili na kuwa na usikivu darasani.

Kwa maana hiyo, kamati za shule zingetakiwa kuwasiliana na wazazi na walezi wa wanafunzi ambao hawajalipa fedha kwa ajili ya kuchangia chakula hicho badala ya kuchukua hatua ya kuwarudisha nyumbani bila ya kuwapa taarifa.

Matokeo yake wanafunzi hao wamekuwa wakitoka nyumbani asubuhi na kuishia mitaani wakijihusisha na vitendo hivyo ambavyo vimekuwa vikichangia kumomonyoka kimaadili.

Watoto hao wanapoamka asubuhi na kuaga wanakwenda shule, wako wanaopewa fedha kwa ajili ya kununua maji, matokeo yake wanaelekeza katika michezo ya kamari, mchezo ambao kwa mujibu wa sheria hauruhusiwi kuchezwa na vijana wenye umri chini ya miaka 18.

Kwa mujibu wa wanasaikolojia, mtoto anapoanza kuwa na akili, ndicho kipindi cha kuanza kumdhibiti kitabia.

Wanasema, akiachwa katika kipindi hicho, ndipo anapoanza kuiga tabia mbaya na njema. Shime wazazi, walezi na walimu tushirikiane katika malezi na makuzi ya watoto kwa kupeana taarifa wanapokuwa shule na nyumbani.

## Rais mpya MAT aanika vipaumbele vyake

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Madaktari Tanzania (MAT), kimesema kwa kipindi cha miaka miwili hadi 2026, kitajikita katika vipaumbele 10, ikiwamo kusimamia weledi na maadili ya wanatasnia hiyo.

Rais wa MAT, Dk. Mugisha Nkoronko, aliiambia Nipashe jana kuwa kipaumbele cha kwanza kwake ni kuendeleza ujenzi wa MAT kwa kusimamia weledi na maadili ya wanachama wake.

Alisema kipaumbele cha pili ni kuwaunganisha wanachama wote, wakubwa kwa wadogo, wa zamani na wa sasa, madaktari mabingwa wabobezi, ili kuunganisha nguvu za kupambana na adui maradhi kwa mtazamo wa kitaaluma.

Dk. Nkoronko alieleza kipaumbele cha tatu ni kuongeza ushirikiano baina ya taasisi kadhaa za ndani na nje ya sekta ya afya za ndani na nje ya nchi.

"Nne, nitaendeleza ushawishi na pengine kwa kutumia mbinu mtambuka na zilizothibitishwa kuleta matokeo makubwa sasa kwa serikali na wadau wa maendeleo kutunga sera na miongozo, inayozingatia maadili na weledi wa taaluma ya udaktari.

"Tano, nitasaidia na kuchangia jitahada za kukuza taaluma ya udaktari kuanzia ngazi za shule za udaktari na sita nitaongeza jitihada za kuelimisha wananchi, ili wajenge tabia njema ya kuzuia magonjwa, kuwahi hospitali wanapoumwa na kuchukua jitihada kwenye tiba za utengamao," alisema Dk. Nkoronko.

Alitaja kipaumbele cha saba kuwa ni kuwahamasisha madaktari kushiriki kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa na wa serikali kuu, mwaka huu na mwakani.

"Kipaumbele cha nane, nitahamasisha ushiriki wa wananchi na wadau wengine kwenye kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu na Agenda 2063 na Dira ya Maendeleo ya Taifa.

"Tisa, pamoja na wadau wengine tutasaidiana kuongeza ushiriki wa madaktari kwenye shughuli za maendeleo, ili kuongeza mchango wa sekta kwenye pato ghafi la taifa.

"Na mwisho, nitachagiza ushirikiano wa sekta binafsi, sekta ya umma na wadau wa maendeleo kujenga taifa lenye huduma bora za afya na zilizo salama," alisema.

Dk. Nkoronko anashika nafasi hiyo baada ya Dk. Deus Ndilanha, aliyeshika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka miwili.



Mufti na Shehe Mkuu wa Tanzania, Shehe Aboubakary Zubery (kushoto), akikabidhi kompyuta mpakato kwa mmoja wa washiriki wa semina ya wiki moja ya ujasiriamali kwa wanawake kutoka mikoa tisa ya Tanzania Bara na Visiwani, iliyoandaliwa na Taasisi ya kiislamu ya TAAWANU, Kigamboni, Dar es Salaam juzi. Wengine ni Mwenyekiti wa Taasisi hiyo, Shehe Hashimu Kamgunda (wa pili kushoto) na viongozi wengine wa taasisi hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wauawa kwa kunyongwa, muuaji awatoboa macho

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WATU wawili wameuawa kwa kunyongwa kwa kamba kisha kutobolewa macho nyumbani kwao katika eneo la barabara ya nne jijini Tanga huku baba mwenye nyumba Alii Bagidad (60) akiwa hajulikani alipo.

Waliouawa ni Saira Mohammed (50) ambaye ni mama mwenye nyumba pamoja na binti wa kazi aliyetajwa kwa jina moja la Asha (20).

Mwandishi wa Nipashe alifika nyumbani kwa marehemu jana na kuzungumza na majirani wa familia hiyo ambao walisema walikuta miili ya wawili hao ikiwa na kamba shingoni huku wakiwa wameingiziwa nguo mdomoni.

"Baada ya jirani mmoja kuja kugonga kwenye hii nyumba na kukuta ukimya, alilazimika kuchungulia ndani ndipo akamwona mama mwenye nyumba yuko chini amelala na ikaonekana miguu ya msichana wa kazi.

"Lakini yule mama alivyokuwa akionekana pale chini, alionekana kama amefariki dunia, ikabidi atafutwe mwenyekiti wa serikali za mitaa, akasema 'haiwezekani kuvunja mlango itabidi tuwatafute polisi'," alisema Halima Shebe, jirani wa familia hiyo.

Aliendelea kusimulia kuwa, "baada ya polisi kufika, walivunja mlango wa mbele na kuingia ndani, akaonekana mama yuko kwenye korido, wakaendelea mbele chumbani wakamkuta dada wa kazi naye amelala chini.

"Polisi walifanya taratibu zao za kutoa ile miili ya marehemu na kuiweka ndani ya gari lakini mpaka sasa hatujui lile tukio wamefanyiwa na nani na baba mwenye nyumba mpaka sasa anatafutwa, hajulikani yuko wapi, simu zake tangu jana hazipatikani. Kwa hiyo, hapa hatujui nani kafanya tukio hilo.

"Lakini yule mama alivyokuwa akionekana pale chini, alionekana kama amefariki dunia, ikabidi atafutwe mwenyekiti wa serikali za mitaa, akasema 'haiwezekani kuvunja mlango ..

"Gari la baba mwenye nyumba lipo hapo nje tangu jana na yeye mwenyewe jana mpaka majira ya saa 10 jioni nimemwona, yaani bado tuna wasiwasi kufuatia jambo hili, tunasubiria polisi wafanye kazi yao."

Mwenyekiti wa Umoja wa Wenyeviti Wilaya ya Tanga, Bunu Omari Bahero alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama kukabiliana na matukio ya kuuawa na kutekwa kwa watu ili jamii iishi bila hofu katika nchi yao.

Jeshi la Polisi Mkoa wa Tanga limethibitisha kutokea mauaji hayo likimtuhumu Bagidad kuhusika na mauaji hayo ingawa hadi jana alikuwa hajulikani alikokuwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa Tanga, Almachius Mchunguzi, alisema juzi kuwa tukio hilo lilitokea Septemba 30 mwaka huu, saa moja usiku.

Kamanda Mchunguzi alitoa wito kwa wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa mahali popote atakapoonekana Bagidad ili akamatwe na sheria ichukue mkondo wake.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Mgambo wadaiwa kumuua kikatili kijana

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MKAZI wa Kijiji cha Muhintiri wilayani Ikungi, mkoani Singida, Frank Joseph Mnyaru (28), anadaiwa kuuawa na askari mgambo kwa kuingiziwa mti sehemu ya haja kubwa katika ofisi ya Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, amethibitisha kutokea kwa mauaji hayo na kwamba kutokana na tukio hilo watu watatu akiwamo Mtendaji wa Kijiji wanashikiliwa na Jeshi la Polisi.

Apson akizungumza jana kwa simu alilaani mauaji hayo ya kinyama na kuwataka viongozi waliopewa mamlaka kutotumia mabavu katika utendaji wao wa kazi na badala yake inapotokea mwananchi amekosea taratibu za kisheria zitumike na sio kumpa kipigo na kumsababishia kifo. "Tanzania ni nchi ya amani tusitumie nafasi zetu vibaya kukandamiza watu, kudhibiti mtu ili asiweze kuleta madhara isiwe na maana ya kumpiga hadi kumuua," alionya Apson ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya hiyo.

Mama mzazi wa kijana aliyeuawa, Caroline Mhango, akizungumza kwa uchungu wakati wa mazishi ya mtoto wake yaliyofanyika juzi kijijini hapo, alisema mwanawe alifikwa na mauti Septemba 29, 2024 wakiwa katika mapokezi kwenye zahanaji ya kijiji cha Ihanja.

Alisema baada ya kupewa taarifa za kupigwa mtoto wake alimfuata Mtendaji wa Kijiji kumuuliza kulikoni na alimjibu kuwa aliwatuma mgambo kwenda kumkamata baada ya kugombana na mwenzake.

Caroline alisema kutokana na kutokwa damu nyingi walimpeleka zahanati kwa ajili ya matibabu, lakini bahati mbaya mauti yalimkuta kabla hajapatiwa matibabu.

**"Tanzania ni nchi ya amani tusitumie nafasi zetu vibaya kukandamiza watu, kudhibiti mtu ili asiweze kuleta madhara isiwe na maana ya kumpiga hadi kumuua," alionya Apson ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi ...**

"Daktari aliyemfanyia uchunguzi alisema kifo cha mwanangu kimetokana na kuchokonolewa na mti kwenye sehemu za siri za haja kubwa, nilimwambia Mtendaji wa Kijiji awajibishe mgambo waliofanya tukio hilo," alisema Caroline huku akionesha majibu ya daktari aliyefanya uchunguzi wa mwili huo.

Mwanakijiji mwingine Idd Shaban, alisema matukio ya wananchi kupigwa na mgambo na vyombo vingine vya usalama na kujeruhiwa vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara katika kijiji hicho, lakini wahusika hawachukuliwi hatua.

Naye Shaban Yusuph, alisema mfululizo wa matukio ya watu kupigwa na kuuawa yanayotokea katika kijiji chao inabidi viongozi waliopo madarakani waachie ngazi kwa madai ya kushindwa kuwajibisha wanaofanya vitendo hivyo.

Nasibu Jumanne, alisema waliohusika katika tukio hilo la mauaji wachukuliwe hatua kali ili iwe fundishe kwa wengine ambao wamekuwa wakitumia madaraka yao vibaya kuumiza wananchi.

Alisema ni jambo la kushangaza kuona vitendo vya kikatili vinafanywa ndani ya ofisi ya serikali na kwamba wakati umefika kwa viongozi kuchukua hatua kali kwa wahusika ili wananchi wawe na imani na serikali yao.

Felister Mhango, mama mkubwa wa marehemu alisema alikuwa wa kwanza kupewa taarifa kwamba Frank (marehemu) hali yake ni mbaya na amepelekwa katika Zahanati ya Ihanja.

Alisema baada ya kufika katika zahanati hiyo alimkuta Frank akiwa peke yake bila mwangalizi na baada ya kuwauliza wahudumu wa zahanati hiyo walisema alipelekwa hapo na mgambo wa kijiji cha Muhintiri na kumtelekeza.




Naibu Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu, Prof. Ezekiel Amri (kushoto), akizungumza wakati akifungua warsha, jijini Dar es Salaam jana, iliyolenga kuunganisha mitaala inayozingatia matokeo na umahiri katika Taasisi za Uhandisi za Elimu ya Juu iliyohusisha vyuo vitano, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Sayansi na Teknolojia (MUST), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na taasisi hiyo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Serikali kuendelea kutoa vibali vya ajira kuondoa upungufu watumishi

**Na Veronica Mwafisi,** MUSOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amesema serikali inaendelea kutoa vibali vya ajira ili kuondokana na adha ya uhaba wa watumishi kutokana na kasi ya ujenzi wa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali nchini ikiwamo ya afya na elimu.

Simbachawene aliyasema hayo jana wakati wa ziara yake ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi katika Mkoa wa Mara ikiwa ni utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

"Katika sekta ya afya, mchakato wa ajira umefanyika kwenye mikoa yote, waombaji wameomba na katika Mkoa wa Mara kama ilivyo katika mikoa mingine, Katibu Tawala wa Mkoa na wasaidizi wake wamesimamia kazi hiyo na watumishi hao wamepatikana hivyo, wanakuja wa kutosha, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amemaliza kazi yake," alisema Simbachawene.

Aidha, katika sekta ya elimu kama ilivyokuwa kwenye afya, mchakato wa ajira utaanza tena na waombaji wataomba tena kupitia kwenye mikoa na huko ndiko watakapangiwa wenyewe sehemu yenye upungufu na sio tena Ofisi ya Rais-Utumishi au Ofisi ya Rais-TAMISEMI kama ilivyokuwa awali.

Simbachawene aliwasisitiza viongozi wa mkoa huo kutokana na taarifa za upungufu wa watumishi kwa kuwa mahitaji ya watumishi yanapangwa kutokana na maombi ya mkoa husika.

"Katibu Tawala wa mkoa, kwenye upungufu wa watumishi tusaidiane kupeana taarifa na kwa wale ambao hawatapatikana kupitia mchakato wa ajira mpya katika mkoa wenu, basi tutafanya uhamisho kwasababu kasi ya maendeleo ni kubwa sana hivyo suala la upungufu wa watumishi ni lazima lipewe kipaumbele."

Simbachawene alitoa wito kwa watumishi wa umma kuhakikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi unakuwa ndio kipaumbele.

# CCM hairidhishwi ujenzi barabara Ifakara - Mbingu

**Na Ashton Balaigwa,** MROGOORO

KAMATI ya Siasa ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Morogoro, imesema haijaridhishwa na mwenendo wa ujenzi wa Barabara ya Ifakara - Mbingu, wilayani Kilombero inayojengwa kwa kiwango cha lami.

Kutoridhishwa kwa kamati hiyo kunatokana na barabara hiyo kutakiwa kuanza ujenzi Desemba 8, 2023 na kutakiwa kukamilika Juni 8, 2026, lakini bado unasuasua.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Joseph Masunga, akizungumza kwa niaba ya wajumbe wa kamati hiyo baada ya kufanya ziara ya kutembelea miradi mbalimbali, alieleza masikitiko yake na kamati mzima kutokana na mradi huo kuendelea kusuasua.

Alisema mradi wa ujenzi wa barabara ya Ifakara-Mbingu ya kilometa 62.5 kwa kiwango cha lami utekelezaji wake bado ni kizungumkuti kwa madai ya kutolipwa malipo ya awali mkandarasi kwa mujibu wa mkataba.

"Napenda kueleza masikitiko yangu kutokana na mradi huu kusuasua, barabara ndio kero kubwa katika maeneo ya Ifakara kwenda Mlimba," alisema Mhandisi Masunga.

Alisema, serikali kupitia Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS), imempa zabuni Mkandarasi wa Kampuni ya M/s Henan Highway Engineering Group Co. Ltd ya Kichina kujenga barabara ya Ifakara-sehemu ya kwanza Ifakara-Mbingu ya kilometa 62.5 kwa kiwango cha lami.

Kutokana na ucheleweshaji huo, Mwenyekiti wa CCM mkoa aliielekeza serikali ngazi ya wilaya na mkoa kufuatilia kwa karibu tatizo hilo ili mkandarasi huyo alipwe na kuanza mara moja ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Mhandisi Masunga alisema barabara hiyo ilileta adha kubwa kwa wananchi wa Mlimba na maeneo mengine hususani wakati wa masika.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema mradi huo uko mikononi mwa TANROADS makao makuu na mkoa na alitaka kujipanga zaidi ili kuhakikisha unaanza kutekelezwa mapema kwa manufaa ya taifa na usafirishaji wa mazao ya wananchi. Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Geofrey Mtakubwa, alisema mpaka sasa kazi zilizofanyika katika mradi huo ni upimaji, ujenzi wa kambi ya mkandarasi na kuleta vifaa 57 kati ya 137 sawa na asilimia 41.6 pamoja na kuleta wataalamu saba kati ya tisa wanaohitajika.

Mhandisi Mtakubwa alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 62.5, inayojengwa kwa kiwango cha lami itakayogharimu Sh. bilioni 97.1 unatekelezwa na mkandarasi M/S Henan Highway Engineering Group ya nchini China na kusimamiwa na TANROADS, ulitakiwa kuanza kutekelezwa Desemba 8, 2023 na kukamilika Juni 6, 2026.

Barabara hiyo ni muhimu kwa wananchi kusafirisha bidhaa zikiwamo za kilimo kutoka maeneo mbalimbali ukiwamo Mkoa wa Morogoro pamoja na Mkoa wa Njombe, kupitia Ifakara, Mlimba, Kihansi hadi Makambako, mkoani Njombe na kukamilika kwa ujenzi huo kutapunguza gharama za usafiri na usafirishaji wa mazao.



# Utalii kupaisha mapato ya serikali mwakani

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI imesema inatarajia kuongeza mapato hadi dola za Marekani bilioni sita katika sekta ya utalii na kufikisha idadi ya watalii milioni tano mwakani.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, alitangaza mpango huo juzi, jijini hapa wakati akifungua Kongamano la Siku ya Utalii Duniani.

"Malengo ya wizara yetu kufika mwaka 2025 tunataka tuwe tumeongeza ukusanyaji wa mapato kufikia zaidi ya Dola za Kimarekani Bilioni sita na watalii zaidi ya milioni tano," alisema Kitandula.

Alisema kwa mwaka jana wamekusanya mapato zaidi ya Dola za Kimarekani Bilioni tatu, kasi hiyo inahakisi uelekeo wa kufikia malengo yao.

"Tunaamini tutafikia lengo na kuvuka mpaka kufikia mwakani kwa kuwa mipango iliyopo ni kuhakikisha tunafungua kanda ambazo bado zilikuwa chini kwa masuala ya kiutalii ikiwamo kanda ya kusini," alisema na kuongeza kuwa:

"Tutahakikisha tunaboresha miundombinu ya viwanja vya ndege, barabara na kutangaza vivutio vilivyoko huko, kwa kuwa itachangia kufikia lengo."

Kwa mujibu wa Kitandula, kwa sasa masoko ya utalii kutoka nchi za Brazil, China na India yamefunguka mbali na masoko yao ya kimkakati ya Ulaya na Marekani.

Alisisitiza kuwa wataendelea kutunza na kuhifadhi rasilimali zilizopo nchini, ikiwamo misitu kwa kuwa vina umuhimu kwa taifa na kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

**Tuna wajibu wa kuhakikisha vyanzo vinahifadhiwa na kutunzwa ili viweze kuwa na manufaa kwa nchi na taifa letu," alisema Naibu Waziri huyo.**

"Tuna wajibu wa kuhakikisha vyanzo vinahifadhiwa na kutunzwa ili viweze kuwa na manufaa kwa nchi na taifa letu," alisema Naibu Waziri huyo.

Vilevile, alisema asilimia 25 ya fedha za kigeni zinazotokana na utalii, asilimia 15 inachangia katika pato la taifa, hivyo kuwa na umuhimu kwa wananchi katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Nawapongeza Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kwa kuona umuhimu wa kuchukua jukumu la kusheherekea Siku ya Utalii Duniani kwa kuwa inasaidia kufungua milango ya ujenzi wa maarifa mapya kwa kuangalia namna nchi yetu itakavyoweza kushirikiana na mataifa mengine kuikuza sekta ya utalii," alisema Kitandula.

Mkuu wa IAA, Profesa Eliamani Sedoyeka, alisema chuo hicho kina vitivo vitano, kati ya hivyo, kimoja kinahusu utalii.

Prof. Sedoyeka, alisema kongamano la maadhimisho hayo, wadau na wanazuoni wamejadili muktadha wa sekta kuanzia ngazi ya masomo na utafiti.

"Sisi kama wadau katika biashara ya utalii kinachouzwa ni uzoefu na katika kufanya hivyo rasilimali watu ni jambo muhimu na IAA tumetengeneza mtaala wa shahada na tunawafundisha wanafunzi kwa vitendo namna ya kuhudumia katika sekta ya utalii," alisema Sedoyeka.



Katibu wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Nachia Juma Ali (kushoto), akikabidhi limu za karatasi kwa Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Nkumba, Pius Hiza jana, kwa ajili ya matumizi ya ofisi, alipokuwa na ujumbe wake wakifanya ziara ya kuwahamasisha wananchi kujitokeza kujiandikisha katika daftari la mkazi kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Neema yazidi kuwashukia wanaohama Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** TANGA

MAMLAKA ya Hifadhi ya Taifa Ngorongoro (NCAA) imesema mradi wa ujenzi wa nyumba 2,500 katika Kijiji cha Msomera kilichoko Kata ya Misima, Handeni, mkoani hapa umekamilika kwa ajili ya kuendelea kupokea wananchi wanaohama kwa hiari Tarafa ya Ngorongoro, mkoani Arusha.

Msimamizi Msaidizi wa Mradi huo, Faudhi Bossa, aliyasema hayo juzi katika Wilaya ya Handeni wakati wa mapokezi ya kaya 26 zenye watu 119 na mifugo 300 zilizokubali kuhama kwa hiari kutoka ndani ya NCAA.

Alitoa taarifa hiyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Albert Msando, aliyewakilishwa na Ofisa Tarafa ya Sindeni, Baraka Nkatura.

"Tumepokea kaya 26 ambazo leo tunawakabidhi makazi yao ikiwa ni nyumba yenye vyumba vitatu iliyojengwa kwenye eneo la hekari 2.5. Nyumba hii ina umeme na tumeweka maji ndoo mbili za kuanzia ili waweze kutumia kwa ajili ya mahitaji yao binafsi," alisema Bossa.

Baada ya kukabidhiwa nyumba yake, akitokea Ngorongoro, Meleji Laitayok, alisema kuwa: "Nimefurahi sana nimepata nyumba nzuri kwa sababu kule Ngorongoro tulikuwa hatuwezi kujenga wala kufanya shughuli za maendeleo, lakini sasa tukiwa huku tunaweza kujiendeleza na kuboresha maisha yetu zaidi."

Daniel Panin kutoka Kijiji cha Nainokanoka, Ngorongoro, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwapa fursa ya kuboresha maisha yao nje ya hifadhi na kuahidi watatumia vyema fursa hiyo kujiendeleza na kuboresha maisha yao.

Ofisa Tarafa Nkatura akizungumza baada ya mapokezi hayo, alisema serikali itahakikisha wananchi hao waliokubali kuhama kwa hiari wanapatiwa huduma bora kama walivyoahidiwa.

"Leo tumewapokea rasmi, mtakabidhiwa makazi yenu mapya yaliyoandaliwa na serikali, ambako mtapewa nyumba yenye vyumba vitatu iliyojengwa kwenye eneo lenye hekari 2.5.

"Kuna maeneo yaliyotengwa mahusus kwa ajili ya shughuli za malisho na kilimo ambayo mtaonyeshwa na wataalamu wetu ndani ya siku chache zijazo," alisema.

Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba za makazi Msomera kwa ajili ya wananchi wanaohama kutoka ndani ya Ngorongoro kwa hiari.

Hadi kufikia Septemba 28 mwaka huu, nyumba 3,003 zimekamilika kwa awamu mbili za ujenzi; na kati ya hizo 1,473 zina watu na nyingine zinasubiri wanaondelea kujiandikisha kuhama kwa hiari kutoka ndani ya hifadhi hiyo.

# Ukatili wa kijinsia bado tishio Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara unatishiwa na ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto, wanawake baada ya kipindi cha miezi minane kuripotiwa 2,099.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa huo ambaye ni Mratibu wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA-II), Anna Fisoo, alisema matukio hayo yameripotiwa kati ya Januari hadi Agosti mwaka huu.

Fisoo alitoa takwimu hizo jana wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Babati Day iliyoko Babati wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya 'Tawaangalie kabla hawajaharibiwa' inayoendeshwa na Jeshi la Polisi na Dawati la Jinsia Mkoa huo.

Aliwataka vijana kutoa taarifa kwa sababu bado kuna vikwazo vya matukio mengi ya ukatili kusuluhishwa kifamilia na kuwakosesha haki zao za msingi kwa mujibu wa sheria.

Kulingana na Fisoo, takwimu za ukatili wa kijinsia zinaendelea kuongezeka na kwamba mwaka jana yaliripotiwa matukio 8,360.

"Yaani bado kuna watu wanamalizana kimila, mtu anapigwa halafu wazee wanakuja wanamalizana wana kula mbuzi; au mtoto amepachikwa mimba wazee wanamalizana na bila kufikiria ndoto za mtoto.

...Naomba wanafunzi vunja ukimya kama kitu ambacho kinakutesa ni vyema ukazungumza ili uwe huru na ukatibiwe na taarifa zako zibaki kuwa siri," alisema Fisoo.

Alisema kwa mujibu wa kanzidata ya mfumo wa afya wa kutolea taarifa zilizowasilishwa Agosti mwaka huu, matukio 6,261 ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto yameripotiwa, huku kwa mwaka jana matukio kama hayo 8,360 yaliripotiwa.

Alilishukuru jeshi hilo hasa dawati la jinsia mkoani humo kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa kusimamia vyema kesi zinazoripotiwa na hukumu kutolewa kama sheria zinavyoelekeza ili kuwa fundisho kwa wengine.

Kamanda wa Polisi wa Manyara, Makarani Ahmed, alisema walengwa wakuu ni wanafunzi wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya kati na vyuo vikuu.

Makarani, alisema wanawatahadharisha kuwa vyuoni kuna wabakaji, walawiti na wasagaji ni kuwajengea uwezo wa kujilinda dhidi ya ukatili.

Mkuu wa Dawati hilo mkoani humo, Willness Kimario, alisema kampeni hiyo inalenga kuibua vitendo vya ukatili vinavyofanyika katika jamii.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Emanuela Kaganda, alisema watu wanaowafanyia ukatili watoto waoga na ndio maana wanawatisha wasisema kwa mtu yeyote.





# 'Wazazi chanzo mmomonyoko maadili kwa watoto'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAZAZI na walezi mkoani Shinyanga wamedaiwa kuwa chanzo cha mmomonyoko wa maadili katika jamii kutokana na malezi mabovu kwa watoto wao hasa wa kike kwa kujiingiza kwenye mapenzi wakiwa na umri mdogo.

Madai hayo yalitolewa juzi na Mwalimu Mstaafu, Catherine Kisula kwenye mahafali ya Shule ya Sekondari ya Rwepa's iliyopo Kata ya Mhungula Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Kisula, alisema wanafunzi wanahitimu masomo wakiwa na nidhamu ila wanapofika mitaani wanabadilika kutokana na mazingira yanayowazunguka.

Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa wakiwaharibu watoto wao hasa wa kike kwa kuwapatia simu janja baada ya kuhitimu elimu ya sekondari au msingi hali inayosababisha kujifunza utandawazi wakiwa na umri mdogo.

Kisula, alisema dunia ya sasa watu wameharibika kwa kufuata baadhi ya mambo ya kwenye mitandao yasiyo na maadili, hivyo wazazi wanatakiwa kuwa makini pindi watoto wanapokuwa na simu zao kwani zimekuwa zikiwafundisha vitu visivyofaa kama mapenzi, ulawiti na ubakaji.

Baadhi ya wahitimu akiwemo Epharahim Hosea, waliahidi kuendeleza maadili mema kwa kutojihusisha kwenye vitendo viovu vitakavyosababisha kujiingiza kwenye makundi hatarishi ya utumiaji wa dawa za kulevya na ulawiti.

Meneja wa Shule hiyo, Frank Samwel, alisema kipaumbele chao cha kwanza ni maadili na taaluma kwa mwanafunzi.

Samwel, alisema hakuna kesi yoyote ya mwanafunzi kupata mimba, ndoa ya utotoni na matumizi ya dawa za kulevya zilizowahi kuripotiwa shuleni hapo.

Mzazi Godfrey Mizengo, alikiri baadhi yao kuwaharibu watoto wao kwa kuwapatia simu janja na kuchangia mmomonyoko wa maadili.

# NEEC yaita vikundi kuchangamkia mikopo

**Na Timothy Itembe,** MARA

BARAZA la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) limevitaka vikundi vya wanawake, vijana, wazee na wenye ulemavu kujisajili katika mfumo wa uwezeshaji watumishi na vikundi ili kutambuliwa na kupata mikopo kutoka serikalini.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa, mjini Musoma wakati wa kuwajengea uwezo kuhusu mwongozo wa kutambuliwa kwenye mfumo wa uwezeshaji watu binafsi na vikundi.

Issa, alisema serikali imekuja na mpango maalum wa kutambua wanachama wa vikundi hivyo kwa lengo la kuwainua kiuchumi na kuwataka wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi kujisajili.

"Hatua hii itawasaidia kujiinua kiuchumi na kupata zabuni, serikali imeelekeza mikopo inayotolewa kwa wanawake asilimia 30 na watapewa kipaumbele wale waliosajili," alisema.

Alisema utoaji wa mikopo kupitia fedha za mapato ya ndani ya halmashauri asilimia 10 kwa makundi maalum, umeandaliwa utaratibu mpya na kuwa katika baadhi ya maeneo itatolewa kwa njia ya benki.

"Niwapongeze vijana wanaofanya shughuli za ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba kwani sekta hiyo imekuwa muhimu katika uhifadhi wa mazingira, pia imekuwa ikiongoza sekta nyingine zinazoombewa mikopo ya asilimia 10," alisema.

**"Niwapongeze vijana wanaofanya shughuli za ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba kwani sekta hiyo imekuwa muhimu katika uhifadhi wa mazingira, pia...**

Ofisa Biashara Mkoa Mara, Gambaliel Timotheo, alisema kupitia elimu waliyoipata wajasiriamali hao ya kujitambua na kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha kutawasaidia kuweka akiba benki.

Timotheo, aliiomba NEEC kuwafikia walengwa hao popote walipo ili wajisajili katika mfumo huo na kunufaika nao kwa kupata mikopo na kuendeleza miradi yao.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya Tarime Vijijini, Anthon Nyange, alisema kujisajili na kukata leseni ya biashara kuvitasaidia vikundi hivyo kutambulika na kupewa mikopo kwa urahisi.

Nyange, alisema halmashauri yake imetenga zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi hivyo.

Alisema serikali imeboresha kundi la vijana kwa sasa umri utakuwa kuanzia miaka 18 hadi miaka 40 na kwa wanawake ni wale ambao maofisa watajiridhisha kwa vigezo vilivyowekwa na serikali kupatiwa mikopo.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, akizungumza na wajasiriamali mkoani Mara juzi, wakati wa mafunzo ya programu ya uwezeshaji kwa wanawake, vijana, wazee na wenye ulemavu inayotekelezwa katika mikoa 13 Tanzania Bara na Visiwani, lengo likiwa ni kuviwezesha vikundi hivyo kujisajili na kupewa mikopo kuwainua kiuchumi. **PICHA: TIMOTHY ITEMBE**

# Wananchi wahofia magonjwa ya milipuko

**Na Remmy Moka,** UKEREWE

WAKAZI wa Kijiji cha Bugombe kilichoko Kata ya Mrutuguru wilayani hapa Mkoa wa Mwanza wameiomba serikali kuboresha miundombinu ya majisafi ili kudhibiti magonjwa ya mlipuko kutokana na kutumia maji ya kwenye visima ambayo si salama kwa afya zao.

Wakazi hao walitoa ombi hilo juzi wakati wa ziara ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Wilaya ya Ukerewe ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Walisema ukosefu wa majisafi na salama katika maeneo yao kusuasua kutokana na kutumia muda mwingi kusaka huduma hiyo kijiji jirani.

Mkazi wa Bugombe, Semeni Busiya, aliiomba serikali kuwafikishia huduma hiyo kwenye maeneo yao ili kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu na kushiriki katika shughuli za maendeleo.

"Licha ya kuwa na maisha duni lakini tumekuwa tukitumia zaidi ya Sh.5,000 kwa siku kwa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na hii ni kutokana na maji hayo kutoka mbali na kijiji chetu," alilalamika.

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Pius Msekwa, Erick Elisha, alisema licha ya shule hiyo kuwa na huduma ya maji taarifa ya kukatika zimekuwa hazitolewi na mamlaka husika na kulazimika kutumia maji ya visima.

Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (MWAUWASA) Kanda ya Nansio, Godfred Mareju, aliahidi kushughulikia maombi hayo ili kuhakikisha maeneo hayo yanapata majisafi na salama.

Kuhusu maji kukatika, Mareju, alisema chanzo ni umeme kukatika mara kwa mara na kusababisha mitambo inayofua maji kutofanya kazi ipasavyo, uhaba wa mabomba na uchache wa mtandao wa usambazaji maji.

Mwenyekiti wa CCM Ukerewe, Ally Mambine, alimtaka mkurugenzi huyo kushughulikia kero hizo kwa wakati na kuwa na utaratibu wa kutoa taarifa za kukosekana kwa huduma hiyo ili kuondoa sintofahamu kwa wananchi.

ama
ALHAMISI OKTOBA 3, 2024
AFYA NA MAZINGIRA







Ukurasa 12

**BINGWA MREMA & UOTESHAJI VIPARA MUHIMBILI:**

KUELEKEA KUMBUKUMBU NYERERE...

# Awamu ya Sita ikitekeleza alichobuni Nyerere 1964, kupitia nyenzo MMAM

**Na Peter Orwa**

KINADHARIA, kitaifa mwaka 1964 unajulikana kuwa msaafu wa taifa, katika mipango mikuu. Ndio Mpango wa Kwanza wa Maendeleo ya Nchi wa miaka mitano.

Ndani yake ilibeba dhana kuu tatu; mwanzo wa kuingia rasmi nchi na mipango yake mikuu; pili kutimizia nchi mahitaji ya msingi kimaendeleo na kimaisha, kabla ya kukwea juu zaidi kimaendeleo.

Pia, sura ya tatu ilinuia kuwahamisha Watanzania kujitegemea kwa kuzalisha na kutumia vya kwao, wakihama kutoka uchumi tegemezi wa 'kuzalisha wasivyotumia na kutumia wasivyozalisha' na badala yake, 'kutumia wanavyozalisha.'



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwapa zawadi kinamama waliojifungua katika jengo jipya la 'Mama na Mtoto' kwenye Hospitali ya CCBRT, Dar es Salaam, Julai, 2022. **PICHA: MAKTABA**

Nne, iliangalia kupiga maendeleo ya haraka kuwaondoa katika hatua ya uchumi wa chini waliokuwa wakati huo kukosa vitu vya msingi, miaka mitatu baada ya uhuru.

Daima hadi sasa mipango yote ya maendeleo inaandaliwa ikiwa na unasaba wa moja kwa moja na mpango huo wa 1964-1969. Mpango huo wa kwanza ulizama zaidi katika huduma za jamii na uchumi, hapo kukizungumziwa sekta za Kilimo, Elimu, Afya, na Ustawi wa Jamii.

Serikali ya Awamu ya Kwanza hadi kutimu miaka 10 ya Uhuru, 1971 kukawapo Mpango wa Maendeleo wa Pili 1969- 1974, ikiwa na sura ya maboresho zaidi katika huduma na mifumo ya uchumi kupanda ngazi, mathalani, kuwapo viwanda vidogo (jukumu la SIDO- 1973) na vya kuzalisha bidhaa nyinginezo za uzalishaji.

Katika afya ikifanana sana na elimu, kukachukuliwa hatua za ziada, kutokana na hali ya chini kimaisha kwa umma uliosababisha na mambo kadhaa.

Hapo kuna upungufu wa zanahati na hospitali, ufahamu duni wa umma katika masuala ya afya, pia katika vifo vya kinamama na watoto na umaskini kwa jumla.

Ni kipindi hata mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile ya afya -WHO na UNICEF kwa elimu na utamaduni yalihamasika sana kufanya kazi na Tanzania.

Kupitia uhamasishaji wa umma wakati huo siasa ya Ujamaa ikitawala hamasa ya nchi na iko rasmi zaidi ya miaka mitano, Serikali ya Awamu ya Kwanza ilipigana kuhamasisha afya, huku ikitekeleza miradi yake mingi nchini.

Ndipo kampeni zake za hamasa kupitia muziki wa dansi bendi kama Morogoro Jazz, zikatunga nyimbo inayohusu afya iliyotamba, wakati huo muziki wa dansi ukiwa katika nafasi yake- burudani ya umma na Radio Tanzania ikitamba kitaifa kufikisha ujumbe mbali.

Kwa wanaokumbuka wakati huo, kundi la watu wasiovaa viatu walikuwa wengi ikiwamo Dar es Salaam, pia wenye funza miguuni, wanaokunywa maji yasiyochemshwa na wanaojifungulia nyumbani nao walikuwa wengi.

Sababu ilikuwa wazi, mfumo wa kikoloni haukujali fursa za elimu ya umma, pia za darasani kwa wazawa wengi, ikizingatiwa utawala wa Kiingereza ulijifahamu ni wa kupita tu (non settlers' colony).

Ndio maana baada ya uhuru katika nafasi ya kipekee, kampeni na hamasa za serikali hasa katika mpango wa kwanza uliokoma mwaka 1969, Rais Julius Nyerere kwa kutumia marafiki aliomba misaada ya ujenzi wa zahanati, pia, kusomeshwa wataalamu kimataifa.

Hapo ndipo ikaanzia hadithi ya kundi kubwa la Watanzania kwenda kusomea utabibu ughaibuni, ikiwamo katika vyuo vikuu vya China na Lumumba, katika iliyokuwa Jamhuri ya Muungano ya Kisovieti (USSR).

Pia Dar es Salaam, ndio katika miaka ya 1960c ukawa mwanzo wa kujengwa zahanati za Mnazi Mmoja, Temeke, Amana na Mwananyamala ambazo sasa ni hospitali kubwa, huku mkoa kama Tanga kuna Zahanati ya Chumbageni, ambayo sasa ni kituo cha afya katika mchakato kama za Dar es Salaam, kuwa hospitali kubwa kimkoa.

Ndani ya Mpango wa Pili wa Maendeleo, operesheni kama za Vijiji vya Ujamaa (1974) mradi wa afya vilihamasisha sana umma kufikiwa na huduma za tiba na katika mtaala maarufu wa elimu mwaka 1976, ulijumuisha somo la Maarifa ya Jamii katika elimu ya msingi, ukiwa ni mwendelezo wa elimu ya afya shuleni.

Daima ni mustakabali ulioendelezwa katika Serikali za Awamu ya Pili chini ya Rais Mzee Ali Hassan Mwinyi na Awamu ya Tatu, Rais Benjamin Mkapa kwa kuwasilisha huduma nyingi za kisekta kwa maeneo hayo, wakipokea na kupokezana kijiti kwa mrithi wake.

**MAGEUZI AWAMU IV**

Ilipotimu Julai 2007, Rais Jakaya Kikwete katika dira ileile ya mwaka 1964 na mwendelezo wa kupokezana vijiti tangu Awamu ya Kwanza, kunuia kumfikia kila mtu ngazi ya msingi au chini, akaanzisha Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM).

INAENDELEA UK.13

AFYA

# BINGWA MREMA NA UOTESHAJI VIPARA MUHIMBILI:

## • Tunatumia puto, tunalijaza miezi minne na linapokua… • Tunavuna nywele kokote, tunapanda kama mpunga. • Upasuaji usiohitaji nusu kaputi, mgonjwa analala 'ana-chati' • Anayeathirika sikio, mkono, mdomo sungura anarekebishwa

**Na Christina Mwakangale**

MATIBABU ya kibingwa yanakua zaidi nchini. Tiba ya upasuaji rekebishi ni miongoni mwake, inayotolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) Kitengo cha Upasuaji Rekebishi na Upasuaji wa Urembo.

Kufanya rekebishi eneo la nje la mwili, zimeongeza takwimu za wanaofika kuhitaji huduma hiyo, wakiwamo wenye vipara.

Mbinu inayotumika kuotesha nywele kwa wenye vipara, wake kwa waume ni kuvuna 'mbegu' (kuvuna nywele kutoka eneo lolote la mwili wa mhusika) na kuipandikiza kama mpunga.

Bingwa wa Upasuaji Rekebishi na Upasuaji Urembo MNH, Dk. Edwin Mrema, aliyasema hayo katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam, kuhusu huduma zinazotolewa na MNH katika kitengo hicho.

Haya ni maswali na majibu kati ya mwandishi wa makala hii na mtaalamu huyo:

**Swali: Unaposema kipara hii inamaanisha nini kitaalamu?**

**Jibu:** Kipara kama tunavyosema kwa Kiswahili ni upungufu wa nywele kwenye kichwa na upungufu wa nywele una sababu tofauti. Upungufu unatokea kote, upande wa kike na kiume.

Ingawa kwa asilimia kubwa unatokea kwa wanaume na sababu zipo tofauti kwanza tunaweza tukarithi kutokana na vinasaba vya familia yako. Umerithi kwa upande wa wazazi, mama, wajomba. Hii ni 'kijenetiki' (genetical).

Au unaweza kupata kipara kutokana na homoni, ukapata kipara baada ya ajali na sehemu ya nywele ikaungua mizizi na kuna sababu zingine hakuna zinazojulikana kisayansi.

Lakini, sababu kama ni homoni, kuna dawa zinatolewa na nywele zikarudi, ila zingine ni hadi upasuaji kama hakuna njia mbadala.

**Swali: Kitengo cha Upasuaji Rekebishi na Upasuaji wa Urembo hapa MNH kilianza lini?**

**Jibu:** Kitengo kina muda mrefu kina miaka takribani 18 hadi 20 tangu kianze na kinakua kwa kasi sasa na taaluma hii inatolewa hapa nchini katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Sasa tuna wanafunzi wa mihula mbalimbali na tunao saba wako darasani na kati ya hao watatu watahitimu mwaka huu, kwenye mahafali yajayo Novemba au Desemba mwaka huu.

**Swali: Tanzania ina wataalamu wangapi hadi sasa wa upasuaji rekebishi na upasuaji wa urembo?**

**Jibu:** Mpaka sasa kuna wataalamu 10 nchini nikiwamo mimi, hivyo kuna uhaba mkubwa kulingana na siku zinavyokwenda tunazidi kuimarika na huduma bobezi zinatolewa ambazo zamani zilitolewa nje.



Bingwa wa Upasuaji Rekebishi na Upasuaji Urembo MNH, Dk. Edwin Mrema. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

Tunaendelea kufundisha na kwenda kutafuta ujuzi ambao hauko hapa nchini, tunaurudisha huku ndani.

**Swali: Mbinu gani zinatumika kuotesha nywele?**

**Jibu:** Kuna njia ya kutumia puto, tunalijaza kwa muda wa miezi minne na linapokua linakuwa na nywele nyingi. Halafu zikiota tunawapandikiza wenye vipara.

Au tukipima damu kliniki kwa kuona homoni hazijawiana tunatoa dawa. Kuna wengine wanapoteza nywele kutokana na sababu za kurithi, hajapata ajali wala kuungua moto.

Hawa tunatumia mbinu ya 'hair transplant' na katika kupandikiza kuna aina mbili zinazohusiana na upasuaji.

**Swali: Nywele au malighafi, mnatoa wapi ili kumpandikiza mtu?**

**Jibu:** Kama mtu ana kipara si pande zote hazina nywele ukimwangalia vizuri mwenye kipara pembeni ya masikio ana nywele kwa mbali.

Swali: Upasuaji wa kupandikiza nywele unafanyika kwa namna ipi?... kama upasuaji mwingine?

Jibu: Ni kama tunavyofanya upasuaji wa aina yoyote, mgonjwa anaingia 'theatre' tunavuna nywele kwa vifaa na kuzipandikiza sehemu ambazo hazina nywele, ila tunazingatia namna mtu huyu nywele zilipoishia.

Unachora unaangalia kwamba huyu nywele zake zitakuwa kwenye 'pattern'(mfumo) hii. Baada ya miezi mitatu na kuendelea nywele zitakuwa zimeanza kuota, tunafanya kwa 'session' (kwa awamu), sio mara moja. Kwa awamu tutahamia upande huu hadi sehemu yote inakamilika.

**Swali: Kipara kinasubiri uzee?**

**Jibu:** Kipara kinaenda na umri. Inategemea kuna wengine wanaanza mapema, akishafikia umri wa kupevuka mapema sana, ila kwa asilimia ndogo. Wengi wanaanza miaka 40 na kuendelea na umri nao kadri unavyokwenda kipara kinakuja.

Wapo ambao wa kurithi, hupata kipara mapema hata kwa umri wa miaka ya 20 anaanza kuwa na 'uwalaza' kama ilivyozoeleka.

> **Wapo ambao wa kurithi, hupata kipara mapema hata kwa umri wa miaka ya 20 anaanza kuwa na 'uwalaza' kama ilivyozoeleka.**

Wengine wanajitahidi 'ku-maintain' (kudumisha) nywele zao, lakini kadri umri unavyokwenda kuanzia umri wa miaka 45 hadi 50 nywele zinaanza kupungua, anakuwa na kipara.

Kuna aina tofauti wengine wanarithi kipara, uzee, ajali!

**Swali: Unapootesha nywele kwa mfumo huo mtu nywele zitarudi kwa kiwango kikubwa au zitakuwa chache?**

**Jibu**: Inategemea na wewe namna ulivyo na asili ya nywele. Tunavuta nywele katika mwili wako mwenyewe, hasa maeneo yenye mafuta, tunavuna 'plasma rich protein' kulingana na mwili wako na kuzianzisha katika 'scalp' hasa kinamama.





Inategemea na huduma, kuna wanaohitaji dawa tu, upasuaji, tunapandikiza.

**Swali: Upasuaji wa kuingia chumba cha upasuaji 'theatre' hutumia saa nyingi?**

**Jibu:** Inachukua saa nyingi, lakini upasuaji ambao utahitaji ganzi kwenye eneo husika. Ni chumba maalum cha upasuaji mdogo. udongo kama kipara na nywele kama mbegu ya mpunga. Ni upasuaji ambao hauhitaji nusu kaputi. Mgonjwa analala tena akiwa macho anachomwa sindano, tena hata akiwa 'ana-chati' tunapandikiza kwenye shina kama mpunga, lakini ukimaanisha.

**Swali: Waliokwishapandikizwa hadi sasa ni wangapi?**

**Jibu:** Hadi sasa tumeshafanyia upandikizaji nywele kwa wagonjwa sita na wanaendelea vizuri, tunawafanyia kwa awamu hadi wakamilishe. Wote ni wanaume.

**Swali: Je, wanaopandikiza kipara wanauchukia mwonekano wao?**

**Jibu:** Kwa ujumla wengi ni mwonekano, kwa sababu kuwa na nywele nyingi ni urembo si kwa wanawake tu, hata kwa wanaume. Ingawa sehemu kubwa wanaona kawaida wanaridhika, anaona amerithi. Mtu anaona ni kama hali ya ujana, kuwa na nywele, anajisikia vibaya kuonekana ameshazeeka, ni kama mtu anakuwa hataki kuonekana na mvi.

'To maintain youthful look' (kuendeleza mwonekano wa kiujana), kwa hiyo wengi ni hiyo na anaona hawezi kuhimili hilo, kuonekana hayuko sawa.

Wengi wanajificha na kofia na wengi wanokwenda ofisini unaweza ukawaona ila kwa ambao wanafanya shughuli zao nyumbani muda wote ni kofia kuficha kipara au mvi. Unaweza usijue kichwa chake, labda watu wa nyumbani mwake.

Na wanaathirika kisaikolojia. Tunafanya huduma hizi kwa kambi kuwakusanya wagonjwa. Huduma ya upasuaji ilianza mwaka jana MNH.

**Swali: Kwako wewe binafsi kwanini taaluma hii uliipenda hasa eneo hili?**

**Jibu:** Hili ni jibu langu binafsi. Binafsi mimi ni bingwa wa upasuaji, ndio shahada yangu ya pili Daktari Bingwa wa Upasuaji, vilevile ni Daktari Bingwa wa Upasuaji Rekebishi na Upasuaji wa Urembo.

Kwa hiyo, baada ya kufanya na kuwa bingwa wa upasuaji, nikaja katika kitengo ambacho kilikuwa kinaanza. Unapofanya 'internship' (mafunzo kwa vitendo) unapita sehemu nyingi kama upasuaji wa watoto, kinamama nikaona ni sehemu hii ninaweza kufanya kazi.

Upasuaji huu ni upasuaji tofauti kama ule watu wanaoujua. Hakuna kitu kinachofurahisha kama mtu anakuja ana shida na ulemavu wa aina fulani alipata ajali, ameathirika sikio, mkono, mdomo wa sungura ukamrekebisha na akarejea kufanya shughuli zake akawa na mwonekano mzuri, ukamsaidia na kesho ukamuona anarejea kwenye shughuli zake, tabasamu inarudi usoni.

Faraja unapata, yaani unafarijika! Yaani ni kitu ambacho kinaonekana nje tofauti na ukiingia tumboni mgonjwa amelala mgonjwa atasema tu asante, ila ndani kulivyokuwa yeye wala mtu mwingine haoni.

Ila upasuaji huu unaonekana nje, kesho unamuona mtu kashika jembe. Tunasaidia kumrejeshea mtu tabasamu lake. Wapo ambao wana majeraha makubwa wanafichwa ndani na hawawezi kutoka nje na jamii ikimwona nastuka.

Haturudishi kama Mungu alivyomuumba lakini, tunamsaidia mtu kuwa na tija, kwake binafsi na jamii.

Kuna wa ajali nyingi ambao wanafika MNH na sisi kitengo hiki lazima tuwapo kwenye kila anayewasili kwa ajali, ili tujue namna ya kurekebisha na ni vizuri kumfanyia upasuaji na anayerekebisha, lakini kila kitengo kinafanya wajibu wake.

Sisi zaidi tunafanya majeraha ya mikono, uso itategemeana na aina ya ajali ukamuacha mgonjwa apate ahueni na nyingine hatusubiri mtu apone tunafanya hapohapo.



Labda ajali za palepale au ajali ziliacha madhara sisi tunarekebisha. Mfano viwandani, ajali za watu waliokatwa mikono, misuli haipati mawasiliano, tutafanyana kazi yetu kuunga misuli kuendesha mikono.

Mfano ajali mfupa uko nje, nyama zimeachwa barabarani na zimechafuka, je, utazipata wapi? Sisi ni wa kufanya 'finishing' wamaliziaji, kuna watu wameondolewa viungo kama saratani ya titi, tunatafuta sehemu ya mwili wako tunakata kipande na kupeleka penye hitaji.

Sisi tunahakikisha mwonekano wa nje unakuwa sawa, wapo watu wana aina fulani ya ulemavu hata wa kuzaliwa nao, ingawa changamoto inabaki katika imani kuna baadhi wanaona kazi ya kuumba ni ya Mungu.

Hivyo kurekebisha haitakiwi, lakini fikiria mtu ameondolewa titi anataka nje huko asijulikane tunamtengezea kitu cha kusawazisha kifuani, lakini hii ni baada ya kujiridhisha saratani seli zote hazitarejea.

Aina, hii ya urekebishi ilianza siku nyingi nchi zilizoendelea ila kwetu ndio inakua, tunahitaji elimu zaidi kwenye jamii. Kwa sababu kama wewe uko sawa, kuna ambao mwonekano unawaletea msongo.

> **To maintain youthful look' (kuendeleza mwonekano wa kijana), kwa hiyo wengi ni hiyo na anaona hawezi kuhimili hilo, kuonekana hayuko sawa.**

**Swali: Kwa muda wa miongo miwili ya kitengo hiki, mahitaji yakoje kwa jamii?**

**Jibu:** Mahitaji ni makubwa na maendeleo yanapokuja matukio yanaongezeka kama ajali kutoka majengo marefu, ajali, idadi ya watu inaongezeka na watu wanazaliwa wengi na ulemavu.

**Swali: Idadi ya wagonjwa wanopokewa kwa siku katika kitengo na wangapi na matukio gani zaidi?**

**Jibu:** Ajali nyingi ni za moto ambazo zinaleta ulemavu. Kuna ajali za viwandani kwenye kemikali, viwanda vya sabuni na chuma, nyumba zinazoungua moto na rufani nyingi zinakuja kwetu, hata ajali nyingi za barabarani mtu kapoteza kiungo wanakuja kwetu.

Kwa siku wagonjwa sita hadi wanane tunawapokea. Upasuaji wa kila siku ni wastani wa wagonjwa 12 hadi 15 kwa wiki. Na sisi tunatumia ubunifu katika kutengeneza mtu na kila mgonjwa upasuaji rekebishi unaweza kutumia saa mbili hadi sita inategemeana.

Kuna upasuaji wa iana tofauti tunaofanya wapo ambao wanapunguza matiti, ameona anataka aonekane vizuri baada ya kunyonyesha watoto, hawaridhiki wanataka matiti yao yasimame na wengine wanataka waongezewe yawe makubwa na wapo wanaotaka kupunguza kitambi baada ya kujifungua.

Wanaume wapo wanaopenda kutengeneza 'six pack' ingawa wanawake wana maeneo mengi ya kufanya upasuaji. Unampunguza mafuta sehemu fulani na mafuta yako unaongezewa kwenye 'hips' au 'body sculpturing au contouring'.

Kuna ambao wana makovu, ngozi zetu (Waafrika) mara nyingi zinaongoza kuwa na makovu. Duniani kuna aina sita za ngozi, Tukiangalia wengi wao duniani kulingana na asili, wanaoongoza kuwa vipara ni 'Whites' (Wazungu), Asians (Waasia), watu weusi (Waafrika) na kwa idadi ya chini sana ni Red Indians (Wahindi Wekundu).

Unapofanya upasuaji unajua mwenye makovu utamfanyia aina gani ya upasuaji.

**Swali: Ni aina gani ya upasuaji ambao umefanya na ni rekebishi ambalo hautasahau?**

**Jibu:** Ni aina za wagonjwa wenye saratani, ili kufanya urekebishi na hata ajali, waliopata ajali viwandani.

## Awamu ya Sita ikitekeleza alichobuni Nyerere 1964

**INATOKA UK.11**

Ni mpango uliokuwa na sura ya maboresho, kuimarisha afya ya umma kuanzia juu hadi chini. Ndani ya tafsiri ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 1964-69 na maboresho yake katika mikakati ya Vijiji vya Ujamaa, MMAM ikataka kila kijiji au kitongoji mijini kuwa na zahanati, huku kata kuwa na kituo cha afya.

Vilevile wilaya inakuwa na hospitali, mkoa hospitali ya rufani, kukawapo hospitali za rufani za kanda kama vile Mbeya na KCMC Moshi na Hospitali ya Taifa Muhimbili, ikiambatana na nyinginezo zenye hadhi kama zake; Benjamin Mkapa (Dodoma), pia Jakaya Kikwete na MOI za Dar es Salaam.

Mbali na ujenzi wake, pia zikaimarishwa vifaa na watumishi wenye stadi ndani yake.

**AWAMU YA SITA**

Katika tafsiri ya msingi ya 'kuchonga penseli' kwa kuendeleza aliyoyakuta, baadhi ya miradi Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akianza nayo awamu ya tano alipokuwa Makamu wa Rais na hata kabla ya hapo, ndio inatoa wasifu Tanzania kung'ara hivi sasa katika stadi za afya.

Sehemu kubwa ya uwekezaji wake, Rais Dk. Samia katika Sekta ya Afya inabeba sura ileile ya mwaka 1964; kuwekeza zaidi katika wataalamu, majengo ya huduma za afya na kampeni za uhamasishaji.

Kuna maeneo amekuwa akiwajibika moja kwa moja, hasa katika huduma zinazohusu 'mama na mtoto' mabako hafichi ukereketwa.

Pia, bajeti kubwa imekuwa ikizama kuendeleza kampeni za elimu afya, wataalamu wa hospitali kubwa kama za JKCI, MNH na Benjamin Mkapa wakipata ujuzi mkubwa ambao uliokuwa haupatikani nchini, mathalan uoteshaji nywele vipara.

Ni aina ya elimu za muda mrefu na mfupi, kuwa sehemu ya bajeti ya nchi kila mwaka na zao lake ni kwamba, ngazi ya ujuzi nchini kwa Afrika Mashariki na wigo wa Afrika umekuwa juu.

Kuna umma wa watu wanaofika nchini kupata huduma tiba iliyokuwa inapatikana mbali kama India, huku wataalamu wa nchi jirani wakifika nchini kupata ujuzi na wale wa Tanzania kwenda kutibu na kutoa mafunzo huko.

Hapo kuna nchi kama vile Malawi, Burundi na Rwanda na kuzalisha aina mpya ya utalii nchini 'Utalii Tiba.'

Vilevile, kuna utaratibu maaluma ya wajuzi hao kuzuri katika hospitali ngazi ya mikoa kupeleka ujuzu huo uwafikie umma uliko. Kwa kifupi sasa, Awamu ya Sita unatekeleza ya mwaka 1964 kwa nyenzo ya MMAM.

msd medical stores department

BOHARI YA DAWA (MSD)

ISO 9001:2015 Certified

# MSD DODOMA YAIMARISHA HUDUMA ZAKE

***Bohari ya Dawa(MSD) ni taasisi iliyoanzishwa kwa Sheria ya MSD Na. 13 ya mwaka 1993 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2021. MSD ina majukumu makuu manne; Uzalishaji, Ununuzi, Utunzaji na Usambazaji wa bidhaa za afya kwenda kwenye vituo vya afya vya umma na vile vya binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya.***

***Dira ya MSD ni kuwa taasisi ya mfano wa kuigwa wa mfumo bora wa ugavi wa bidhaa za afya barani Afrika, huku Dhima yake ni kuwezesha upatikanaji wa bidhaa za afya zenye ubora na toshelevu kwenye vituo vyote vya umma vya kutolea huduma za afya nchini na nje ya Tanzania. MSD ina kanda kumi (10) ambazo ni Kilimanjaro, Mwanza, Tabora, Dodoma, Iringa, Mbeya, Mtwara, Kagera na Dar es Salaam.***

***Katika Makala hii fupi leo tunakutana na Meneja wa MSD Kanda ya Dodoma, Bi Mwanashehe Jumaa, ambaye ameongoza Kanda hiyo mara mbili katika vipindi tofauti.***
==============

**Swali: Kanda ya Bohari ya Dawa (MSD) Dodoma inahudumia maeneo gani?**

**Mwanashehe Jumaa:** Kanda ya MSD Dodoma inahudumia vituo vya kutolea huduma za afya vya Halmashauri zote za Mikoa ya Dodoma na Singida, pamoja na Halmashauri moja ya Kiteto iliyoko Mkoani Manyara.

**Swali: Wateja wenu ni wa aina gani na mnawasiliana vipi kukamilisha mnyororo mzima wa ugavi?**

**Mwanashehe Juma:** Wateja wetu ni vituo vya kutolea huduma za Afya vya umma na vya mashirika ya Dini vilivyoidhinishwa na Wizara ya Afya. Wateja hawa ni wa kutoka vituo vya kutolea huduma za afya vya ngazi zote kuanzia Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda na Hospitali maalum.



*Meneja kanda MSD Dodoma Mwanashehe Jumaa akizungumza na Vyombo vya habari ofisini kwake hivi Karibuni*

Tunawasiliana na wateja wetu kwa njia ya barua, simu, barua pepe, mikutano ya wadau, kuwatembelea wateja. Hata hivyo, tunao mfumo wa kimtandao unaojulikana kwa jina la Customer Porto ambao pia hutumiwa na wateja wetu kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na hali ya upatikanaji wa bidhaa za Afya, kujua hatua maombi yake yalipofikia, kupata taarifa za fedha kwenye akaunti zao zilizoko Bohari ya Dawa, Kuweza kuandaa control number pale wanapotaka kufanya malipo ya bidhaa za Afya.

**Swali: Ni wapi ambapo mmefanya vizuri katika mwaka wa fedha uliopita 2023/2024?**

Mwanashehe Jumaa: Maeneo tuliyofanya vizuri kwa mwaka wa fedha uliopita ni pamoja na kufanikisha kusambaza bidhaa za afya kwa wateja wetu kwa mizunguko yote sita kama inavyotakiwa kwa mujibu wa kalenda ya usambazaji, lakini pia tumeweza kufikia malengo ya mauzo kwa asilimia 107 ya lengo lililowekwa kwa kanda.

Kwa Kanda ya MSD Dodoma katika mwa wa fedha uliopita tumeweza kukusanya fedha taslimu kwa asilimia 66 ya lengo, kupunguza uwezekano wa bidhaa za Afya kuchotora ama kwa neno jingine ni kuchina. Kanda ya MSD Dodoma pia imeweza kusambaza vifaa tiba kwa vituo vya Afya kwa fedha



*Sehemu ya mzigo wa dawa uliohifadhiwa katika bohari kuu ya dawa (MSD) kanda ya kati kwa ajili ya kusambazwa katika maeneo mbalimbali nchini.*

Inaendelea uk 15

*Inatoka uk 14*

imeweza kusambaza vifaa tiba kwa vituo vya Afya kwa fedha ya ruzuku kwa asilimia 50.

Mbali na hayo, Kanda ya Dodoma ilifanya mkutano wa mwaka wa wadau kwa wateja na wadau wa Kanda ya Dodoma na kwa pamoja kujadili namna ya kuendelea kuboresha shughuli nzima za mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya nchini, aidha tumeweza kukaa na hospitali zetu za Rufaa na Hospitali maalum na kuweka mikakati ya kuboresha upatikanaji wa bidhaa za afya.

Pamoja na mafanikio hayo, pia Kanda ya Dodoma tuliweza kukaa pamoja na kufanya tathmini ya mwaka wa fedha uliopita na kupanga mikakati ya utendaji kwa ajili ya mwaka wa fedha 2024/2025.Hata hivyo, kama Meneja wa Kanda niliweza kutambua mchango wa kila kitengo kwa mafanikio ya Kanda ya Dodoma kwa kuwapatia vyeti na tuzo. Pia niliweza kutoa tuzo kwa Menejimenti ya Bohari ya Dawa kwa miongozo na usimamizi wa karibu waliotupatia.

**Swali: Kanda ya Dodoma imejipangaje kuhakikisha inatoa huduma bora zaidi?**

**Mwanashehe Jumaa:** Katika kuhakikisha kanda ya Dodoma inatoa huduma bora imejipanga kuimarisha mawasiliano na wadau na wateja wote, kushiriki vikao kazi vinavyofanyika kwenye Halmshauri na vikiwashirikisha watumishi na wataalam wa vituo vya kutolea huduma za afya kwenye Halmashuri na kupata mahitaji yenye uhalisia kutoka kwa wateja wetu kukwepa kukosekana ama kuwa na bidhaa zaidi ya mahitaji na kusababisha dawa kuchotora. Pia kukaa na wateja wakubwa kuandaa mahitaji na kujadili namna ya kuimarisha mnyororo wa ugavi.

Kwa kuwa wateja wetu wanatakiwa kuridhika na huduma zetu, tutawafikia kwa kuwatembelea kwa asilimia 50% ili kujadiliana namna ya kuboresha huduma na upatikanaji wa bidhaa za Afya.



*Muonekano wa Ghala Jipya ambao unaendelea kujengwa unakaribia kumalizika mwezi November mwaka huu*

**Swali: Kanda ya MSD Dodoma linajengwa ghala la kimkakati, nini faida ya ghala hili kuwepo hapa?**

**Mwanashehe Jumaa:** Uwepo wa ghala la kimkakati Kanda ya Dodoma kuna faida kubwa si tu kwa Kanda ya Dodoma lakini kwa Kanda zilizo jirani na Kanda ya Dodoma kama Tabora, Iringa, Mwanza na Kagera. Faida hizo ni pamoja na Kanda itakuwa inapokea bidhaa moja kwa moja kutoka kwa washitiri na wazalishaji, hivyo kutakuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa toshelevu kwa wateja wanaopata huduma kupitia Kanda ya Dodoma Ghala hilo la kimkakati pia litapunguza umbali wa kufuata bidhaa ghala la Kati, lilipo Dar es Salaam kwa Kanda za Dodoma yenyewe,Tabora, Mwanza, Iringa na Kagera na pia kuongezeka kwa eneo la uhifadhi kwa jumla ya ukubwa wa mita za mraba 7,200 hivyo kulipunguzia msongamano ghala Kuu la Kati yaani ghala lililoko makao makuu.

Katika kuendelea kuboresha huduma za afya nchini serikali ya awamu ya sita kupitia Bohari ya Dawa imewezesha upatikanaji wa vifaa tiba na mashine katika ngazi mbalimbali za vituo vya kutolea huduma za afya nchini. MSD Kanda Ya Dodoma imefanikiwa kusambaza vifaa tiba kwa vituo vya kutolea huduma za Afya vinavyohudumiwa na Kanda hii.




*Watumishi wa MSD Dodoma wakipakia bidhaa za afya tayari kwenda vituo vya kutolea huduma za afya*

Vituo vilivyopata vifaa tiba ni vituo vipya na vile vilivyopandishwa hadhi ya kutoa huduma na kuwa Vituo vya Afya kama ifuatavyo;

Tumeweza kusambaza vifaa vya chumba cha upasuaji, huduma za meno na jokofu la kuhifadhia maiti katika ya Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa. Katika kituo cha afya Sepuka, Katika Halmshauri ya wilaya ya Ikungi, MSD Kanda ya Dodoma tumesambaza mashine ya ultrasound, kiti kwa ajili ya huduma ya Afya ya Kinywa na meno na jokofu la kuhifadhia maiti na hivyo kuwapunguzia wananchi kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hizi Singida mjini.

Katika zahanati ya Shelui, iliyopo Halmashauri ya Iramba, Bohari ya Dawa Kanda Ya Dodoma tumefanikiwa kusambaza vifaa kwa ajili ya jengo la upasuaji na hivyo kuboresha huduma za upasuaji hasa kwa mama wajawazito waliokuwa wanatembea umbali umbali mrefu kufuata huduma katika hospitali ya wilaya ya Kiomboi.

Katika kituo cha afya Mkonze na Hombolo vilivyopo katika jiji la Dodoma tumefanikiwa kuwapatia majokofu ya kuhifadhia miili na hivyo kuwasaidia wananchi kutofuata huduma hizi mjini katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma. Katika kituo cha afya kibaigwa, Kongwa DC tumefanikiwa kusambaza mashine ya kidijitali ya Mionzi, hivyo kuwasaidia wananchi wa kibaigwa kutosafiri kwenda kufuata huduma hiyo katika hospitali ya wilaya ya Kongwa. Katika awamu hii ya sita tunaona maboresho makubwa katika huduma za afya nchini haya ni baadhi tu kwani kanda ya Dodoma pia vituo vimeongezeka vya kutolea huduma za afya na tayari tumekwisha anza kusambaza vifaa tiba kwa vituo vipya vya Mazengo halmashauri ya Chamwino, Msembeta,Soweto na Nkuhungu vyote hivi vipo Dodoma jiji.





# Machifu wapaza sauti mito kukauka

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa mila katika Kata ya Santilia wilayani hapa, Mkoa wa Mbeya, wameomba kushirikiana na taasisi za serikali kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji ili kunusuru mito kukauka baada ya kuvamiwa kutokana na shughuli za kibinadamu.

Wamesema vyanzo vingi vya maji vilivyoko kwenye maeneo yao vimevamiwa na baadhi ya wananchi kwa kilimo, ufugaji na ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa na kusababisha maji kupungua.

Viongozi hao waliwasilisha ombi hilo juzi wakati wa Ziara ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya katika kata hiyo kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza kero za wananchi.

Mmoja wa viongozi hao, Robert Mwaluanda, alisema kwenye eneo lao mto kwa miaka ya nyuma ulikuwa na maji mengi, lakini kwa sasa yamepungua kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa na baadhi ya watu.

Mwaluanda, alisema viongozi wa baadhi ya vijiji vya kata hiyo wamekuwa wakikodisha mashamba kwenye vyanzo vya maji kwa ajili ya kilimo bila ya kuzingatia utunzaji wa mazingira.

"Wanakodisha mashamba kwa ajili ya kupata mapato ya kijiji, lakini wanatuathiri sisi, mto huu kwa sasa unaelekea kukauka kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira huko juu, tunaomba mtusaidie kuwadhibiti," alisema.

> **"Wanakodisha mashamba kwa ajili ya kupata mapato ya kijiji, lakini wanatuathiri sisi, mto huu kwa sasa unaelekea kukauka kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira huko juu...**

Evance Mwaluanda, alisema ili kuwadhibiti waharibifu wa mazingira, serikali inatakiwa kuwashirikisha kwa kuwa wako jirani zaidi na wananchi na wanasikilizwa wanapotoa maagizo.

Alisema misitu inayohifadhiwa na viongozi hao haiharibiwi kama ya serikali kutokana na kukosa usimamizi.

Alisema wao hawalindi misitu kwa kutumia silaha na haiharibiwi, lakini ya serikali ambayo watu wameajiriwa na kuwezeshwa vifaa na kulipwa mishahara inaongoza kwa kuharibiwa.

Baada ya kusikiliza kero hiyo iliyoibuliwa na viongozi hao, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, kutumia vyombo vyake kuwadhibiti waharibifu wa mazingira katika wilaya hiyo. Homera, alisema uharibifu wa mazingira unaofanywa na watu hao unasababisha mabadiliko ya tabianchi, upungufu wa mvua na ongezeko la joto katika maeneo hayo.

"Shirikianeni na watu wote ambao mnahisi watawasaidia kutunza mazingira, fanyeni operesheni za mara kwa mara kwenye maeneo yote na muwachukulie hatua wanaoharibu mazingira," alisema.

Alisema waathirika wa kwanza wa uharibifu huo ni wananchi wa eneo hilo na viumbe wengine.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (katikati), akiongoza wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa huo pamoja na baadhi ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakielekea kukagua vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Santilia, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Watoto wa kike wakombolewa ajira za ndani

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

MWAMKO miongoni mwa jamii mkoani Njombe kwa watoto wa kike kupata elimu, umewaondolea adha ya kwenda kutumikishwa katika kazi za ndani mikoa mingine hususani jijini Dar es Salaam, imefahamika.

Hayo yalisemwa juzi na Mtaalamu wa Masuala ya Jamii kutoka Benki ya Dunia Dk. Naima Besta, wakati wa ukaguzi shirikishi wa miradi inayotekelezwa chini programu ya Mradi wa Kuimarisha Elimu ya Msingi (BOOST) na wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa Halmashauri ya Mji wa Njombe na ya Wilaya ya Wanging'ombe.

Dk. Besta, aliwapongeza wakazi wa Kijiji cha Usalule wilayani Waging'ombe kwa kutoa eneo bure kwa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Njombe ya mchepuo wa sayansi kwa thamani ya Sh. bilioni 4.45 kwa kutambua umuhimu wa watoto wa kike kupata elimu.

Alisema uwepo wa shule hiyo mkoani humo kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, utasaidia kupunguza watoto wa kike kwenda kutumikishwa kazi na kuwasababishia madhara kulingana na umri wao.

"Siku za nyuma mkoa huu wa Njombe, Iringa huku nyanda za juu kusini ni maeneo ambayo yalikuwa yanatoa watoto kwenda kufanyishwa kazi maeneo mengi nchini ikiwamo Dar es Salaam," alisema Besta.

Mratibu Msaidizi wa SEQUIP Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Robert Msigwa, alisema mradi huo unagharama Sh. trilioni 1.2 kwa ufadhiliwa na benki hiyo na kutekelezwa na serikali.

Msigwa, alisema serikali imepiga hatua kuhakikisha inaboresha mazingira ya mtoto wa kike kupata elimu.

Alisema upande wa watoto wa kiume mwaka huu wa fedha, serikali imepeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule za wavulana za kikanda za bweni.

Mratibu wa BOOST wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Lawrence Mselenga, alisema utaratibu wa miradi hiyo pacha ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa pamoja kati ya serikali na benki hiyo katika maeneo matatu.

"Eneo la kwanza ni maeneo ya afua za mradi, eneo la pili kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha na manunuzi ya vitu, eneo la tatu ndilo ambalo limetuleta Njombe ni la ufuatiliaji na uzingatiaji wa uhifadhi wa mazingira na mambo ya kijamii katika miradi ya ujenzi," alisema Mselenga.

Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Joseph Masasi, alisema ujenzi wa mradi wa Shule ya Sekondari Wasichana Njombe ambao umefikia asilimia 92 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka huu.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Njombe, Nelasi Mulungu, alisema kwa mwaka wa fedha uliopita kwa BOOST wamepokea bilioni 6.9 na SEQUIP bilioni 16.8.

# Wasimamizi uchaguzi waagizwa kuzingatia sheria

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WASIMAMIZI wasaidizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya wameagizwa kuzingatia sheria na miongozo ili ufanyike kwa amani na taifa kuwapata viongozi watakaowaletea wananchi maendeleo.

Mwanasheria wa Jiji hilo, Davis Mbembela alitoa agizo hilo juzi wakati akiwaapisha wasimamizi hao ambao ni maofisa watendaji wa kata na mitaa.

Mbembela aliwataka kusoma sheria na kanuni za uchaguzi huo na kuwasiliana na msimamizi wa uchaguzi kupata ufafanuzi wa jambo ambalo hawalielewi ili kuepuka kuharibu uchaguzi.

Alisema pia viongozi hao wanatakiwa kuzingatia kiapo ili kuepuka kukumbana na mkono wa sheria endapo watakiuka kiapo hicho.

"Mmeshapitishwa kwenye taratibu zote za uchaguzi huu, naomba mkazingatie hayo yote ili msiharibu mchakato," alisema Mbembela.

Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi wa Jiji hilo, Ali Nnduma, alisema uchaguzi huo wa serikali za mitaa utafanyika katika mitaa 181 na mpaka sasa vituo vitakavyotumika kupigia kura vipo 210.

Nnduma, alisema kwa mujibu wa utaratibu wa uchaguzi huo, kila mwananchi mwenye sifa, atatakiwa kupigia kura kwenye kituo alichojiandikisha huku akisisitiza kuwa majina yatabandikwa kwenye vituo mbalimbali.

Alisema serikali iliamua kuanza maandalizi mapema ili kuondoa matatizo ambayo yanaweza yakaibuka wakati wa uchaguzi huo ikiwamo wapigakura kuchanganya vituo vyao.

"Tumeanza kwanza kutoa elimu kwa wasimamizi hawa pamoja nanyi wanahabari ili kila mmoja awe na uelewa wa kutosha na tunaomba mtusaidie kueneza elimu hii kwa wananchi wetu," alisema Nnduma.

Baadhi ya wasimamizi ngazi ya mitaa, waliahidi kutekeleza maelekezo ya wataalamu wakati wa mafunzo ili kuhakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa uwazi na haki.

Mmoja wa wasimamizi hao, Lilian Mwakitose ambaye ni Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Pambogo Kata ya Iyela, alisema uchaguzi huo unatoa hatima ya mwelekeo wa taifa.

Aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano kuanzia hatua za awali mpaka watakapotangaza washindi.

## Simu, kompyuta kutumika uboreshaji taarifa mpigakura

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imesema imeboresha mfumo wa uandikishaji ambao kwa sasa utamwezesha mpigakura kufanya maboresho ya taarifa zake kwa kutumia simu ya kiganjani au kompyuta.

Mjumbe wa tume hiyo ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu, Asina Abdallah Omar alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa tume hiyo kwa wadau wa uchaguzi.

Alisema wanaotumia simu zisizo janja nao wanaweza kutumia huduma hiyo na kupata maelekezo pamoja na taarifa zao.

Alisema mzunguko wa sita wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Mpigakura unatarajiwa kuanza Oktoba saba hadi 13 mwaka huu kwa visiwa vya Unguja na Pemba.

"Uboreshaji huu kama ilivyokuwa wa mwaka 2015 na 2020 utahusisha matumizi ya teknolojia ambapo hutumika katika kumtambua mtu na kumtofautisha na mwingine. Unahusisha uchukuaji wa alama za vidole vya mikono, picha na saini na kuhifadhiwa kwenye kanzidata ya wapigakura," alisema Jaji Asina.

Alisema uboreshaji huo ni tofauti na wa miaka iliyopita ambapo kwa mwaka huu utatumia teknolojia ya BVR kits zilizoboreshwa kwa kuwekewa programu endeshi ya kisasa zaidi.

Aidha, alisema kujiandikisha kuwa mpigakura zaidi ya mara moja ni kosa la kisheria kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 114(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Namba 1 ya mwaka 2024.

Alisema kifungo hicho kinaeleza kuwa mtu yeyote atakayeomba kuandikishwa zaidi ya mara moja atakuwa ametenda kosa la kisheria na akikutwa hatiani adhabu yake ni faini isiyopungua Sh. 100,000 na isiyozidi Sh. 300,000 au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili gerezani au vyote kwa pamoja.

Alisema tume imeweka utaratibu kwa watu wenye ulemavu, wazee, wagonjwa, wajawazito na kinamama wenye watoto wachanga watakaokwenda vituoni kupewa fursa ya kuhudumiwa bila kupanga foleni.

Hivyo, aliwataka wadau wa uchaguzi kuwafahamisha wananchi wenye sifa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha au koboresha taarifa zao vituoni kwa kuwa utaratibu mzuri wa kuwahudumia umewekwa.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa INEC, Kailima Ramadhani, alisema uboreshaji wa taarifa nchini unatarajia kukamilika Machi mwakani.

Alisema itahusisha mambo mbalimbali ikiwamo kutoa kadi mpya, waliopoteza kadi au kadi kuharibika, kuondoa wapigakura waliokosa sifa kutokana na sababu mbalimbali.

Aidha, alisema wapigakura 5,586,433 wapya wanatarajiwa kuandikishwa sawa na asilimia 18.7 ya wapigakura 29,754,699 waliopo kwenye daftari.

# INEC yasisitiza weledi uboreshaji daftari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAJI wa Mahakama Kuu na Mjumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Asina Omari, amewataka watendaji ngazi ya mkoa watakaoshiriki kazi za uboreshaji wa Daftari la Wapigakura kufanya majukumu yao kwa weledi, ili kufanikisha uchaguzi mkuu.

Alitoa wito huo visiwani Zanzibar wakati akifungua mafunzo kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa watendaji hao kutoka mikoa ya Unguja.

Alisema mafunzo hayo yalihusisha maofisa waandikishaji na wasaidizi ngazi ya jimbo, maofisa uchaguzi na maofisa wa TEHAMA wa wilaya.

Jaji Asina alisema mafunzo hayo ni muhimu na yatawawezesha kutekeleza majukumu yao ili kufanikisha uboreshaji wa daftari.

Alisema mafunzo hayo pia yatawajengea uelewa wa pamoja utakaowapa fursa ya kutumia kwa ufasaha mfumo pamoja vifaa vingine vya kuandisha wapigakura.

Hivyo, aliwataka mawakala au viongozi wa vyama vya siasa kutoingilia mchakato wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura kituoni na kwamba jukumu lao la msingi ni kutambua waombaji wa eneo la msingi.

Alisema tume imetoa kibali cha kutoa elimu ya mpigakura wakati wa uboreshaji wa daftari kwa asasi za kiraia 157 na asasi za kiraia 34 kwa ajili ya uangalizi, hivyo ni vyema kwa watendaji wakatoa ushirikiano kwa asasi hizo zinapofika kwenye maeneo husika.

Kadhalika, aliwataka watendaji kutekeleza majukumu yao kwa umakini katika kila eneo ikiwamo utunzaji wa vifaa vya uandikishaji.

Alisema matokeo bora ya zoezi hilo yanategemea uwepo wa ushirikiano mkubwa kati ya watendaji wote wa uboreshaji, serikali, vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi.



Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Said Ali Muhamed, akizungumza na waandishi wa habari, mjini Zanzibar jana, wakati akitoa taarifa kuhusu makusanyo ya kodi kwa mwezi wa Septemba mwaka huu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Samia: Serikali, sekta binafsi mshirikiane uboreshaji afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kuna umuhimu kwa serikali kushirikiana na sekta binafsi katika kutoa huduma bora za afya kwa wananchi, ili kusaidia kuondoa changamoto katika upatikanaji wa matibabu.

Alisema bado sekta hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uhaba wa wafanyakazi wenye ujuzi, upungufu wa vifaa tiba na uchakavu kwa baadhi ya miundombinu.

Aliyasema hayo katika hotuba yake iliyosomwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, wakati wa ufunguzi wa Kongamano la 11 la Tanzania Health Summitt (THS) na kuwakutanisha wataalamu wa afya zaidi ya 1,500.

Alisema serikali itaendelea kuboresha elimu kwa wataalamu wa afya kwa kutoa kipaumbele na kuongeza ufadhili kwa mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi katika taaluma za kimkakati.

Aidha, alisema serikali zote mbili ya SJMT na SMZ zinaendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya utoaji wa taarifa ili iweze kusomana kutoka kituo kimoja cha afya kwenda kingine.

Alisema pamoja na hatua zinazofikiwa bado kuna changamoto katika utoaji wa huduma, hivyo serikali itaendelea kushirikisha sekta binafsi katika kutoa huduma kwa wananchi.

Akizungumza kwa niaba ya Bodi ya Tanzania Health Summitt, Dk. Grace Magembe alisema THS ni chachu ya kuleta mabadiliko endelevu katika sekta ya afya, hususani katika kuhamasisha utoaji wa huduma kwa mifumo ya kidijitali ili kuendana na wakati.

Dk. Grace alisema THS imewawezesha vijana kupitia programu ya Youth Capacity Building kwa kuwapatia mafunzo, kuwaendeleza kitaaluma pamoja na kuwaunganisha watumishi wa afya na fursa mbalimbali zilizopo nje ya nchi.

Waziri wa Afya, Jenista Mhagama alizikaribisha sekta binafsi kushirikiana na serikali katika kujenga huduma za kibingwa ili kuifanya Tanzania kuwa kituo cha utalii wa afya kama yalivyo maeneo mengine.

Alisema bado serikali inahitaji ushirikiano mkubwa na sekta binafsi katika maeneo mbalimbali na serikali ipo tayari katika hilo, kwamba itakachofanya ni kuboresha mifumo katika ushirikiano huo.

Kuhusu bima ya afya kwa wote, Mhagama alisema kwa sasa sekta binafsi inapaswa kushirikiana na serikali kuhakikisha lengo la kutoa huduma nzuri na rahisi kwa wananchi zinafanikiwa.

Waziri wa Afya Zanzibar, Ahmed Mazrui, alisema ubia wa sekta binafsi ni mkubwa na wenye mafanikio makubwa katika uboreshaji wa miundombinu ya vifaa tiba vya kisasa.

Alisema licha ya kuwapo changamoto kadhaa lakini serikali inaendelea kushughulikiwa.

Mazrui alisema kwa sasa wanaimarisha vituo vya afya vya msingi 52 na kujenga vipya 96 ili ifikapo mwakani huduma za afya ziwe bora zaidi kwa wananchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SUZAN. S. RWEYEMAMU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1372-0068** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KIWANGWA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **9910886842392**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FREDNAND D. MAMCHONI** anatangaza kupotea kwa cheti kidato cha nne chenye index namba **S0782-0176** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MWIKA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2009. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/52332/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAMADHANI MOHAMED HOTTI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3790/0076** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAFISA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/213397/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**ALEX JULIUS NYAMHANGA** naomba kutangaza kupolewa na hati yangu ya kusafiria yenye namba **TAE778418** iliyotolewa uhamiaji makao makuu mnamo tarehe 13/september/2024. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/213554/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **ARNOLD ELIFURAHA MAEDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye namba za usajili **T 901 ABR.** Na chassis No.**LH70V000355,** pamoja na Engine No. **3Y0018966.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Amefika Polisi na amepewa Loss Report. Taarifa Polisi: **PAN/RB/818/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FREDRICK FAUSTIN KOMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 340 CJS – TOYOTA PASSO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/213412/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU RAMADHAN MOHAMMED JUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T421 DGN** aina ya **BMW X3** rangi Nyeusi. Kwa yeyote atakayefanikiwa kuiona kadi hiyo atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu naye. Taarifa ya Polisi namba **PHQ/DOD/DOD/43938/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI AT KINONDONI**

**COMMERCIAL CASE NO. 5106 OF 2024**

**BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED...PLAINTIFF**

**VERSUS**

**WITNESS ROBINSON SHOO..............DEFENDANT**

**TO: WIITNESS ROBINSON SHOO**

**NOTICE DATE FOR EXPARTE JUDGMENT**

**THE NOTICE** that the above case has been fixed for **EXPARTE JUDGMENT** on 17th day of OCTOBER 2024 at 09:00 a.m. Before **Hon. V. KASEKO – SRM YOU ARE** required to appear in this Court without failing.
Given under my Hand and the Seal of the Court this **25th day of SEPTEMBER 2024**

V.KASEKO, SRM

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI,

KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Iran yapiga makombora 180 Israel

**TEHRAN,** Iran

IRAN imeishambulia Israel kwa makombora 180 na kuchochea mzozo wa miezi kadhaa baina ya Israel na makundi yanayoungwa mkono na Iran ya Hamas na Hezbollah.

Msemaji wa jeshi la Israel, Daniel Hagari alisema kuwa shambulizi la makombora hayo lililofanywa na Iran jana likilenga kuwaua maelfu ya watu wa Israel na halikuwa la kawaida na wala halikutarajiwa.

Jeshi la Israel lililaani shambulizi hilo likiliita kuwa ongezeko baya na la hatari la machafuko, huku Hagari ikisema Iran na washirika wake wanataka kuiangamiza Israel na kutakuwa na matokeo na hatua za kujibu shambulizi hilo.

Rais wa Marekani, Joe Biden alisema wanaiunga mkono kikamilifu Israel kufuatia shambulizi hilo la makombora ya masafa marefu, akilieleza kuwa limeshindwa na lisilo na tija yoyote.

**Kauli zisizoeleweka za ikulu ya Marekani zinaonyesha kuwa taifa hilo liko katika hali ya kutokuwa na msaada kabisa katika kuitafutia ufumbuzi migogoro.**

Akizungumza na waandishi wa habari katika ikulu yake mjini Washington, Biden alisema kuna mazungumzo yanayoendelea kuhusu jinsi Israel itakavyojibu shambulizi la Iran na kwamba athari kwa serikali ya mjini Tehran zitaonekana. Na kwamba atazungumza na Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu.

Wakati huo huo, Russia ilisema sera ya Marekani kuelekea Mashariki ya Kati imeshindwa kabisa. Huku Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa taifa hilo Maria Zakharova akisema utawala wa Rais Biden umefeli Mashariki ya Kati na kinachoendelea ni tamthilia ya umwagaji damu inayoendelea kushika kasi.

Aliongeza kuwa kauli zisizoeleweka za ikulu ya Marekani zinaonyesha kuwa taifa hilo liko katika hali ya kutokuwa na msaada kabisa katika kuitafutia ufumbuzi migogoro.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran ililitaka Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lichukue hatua za maana kuepusha vitisho dhidi ya amani na usalama wa Mashariki ya Kati.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa baraza la usalama litafanya kikao cha dharura kujadili ongezeko la machafuko Mashariki ya Kati, huku Msemaji wa ofisi ya balozi wa Uswiwi katika Umoja wa Mataifa, nchi ambayo inashikilia urais wa baraza la usalama la umoja huo, akisema Uswisi imeshapanga muda wa kikao hicho kufanyika.

Umoja wa Ulaya (EU) umetoa wito wa kusitisha mapigano mara moja Mashariki ya Kati.

Mkuu wa sera za kigeni wa umoja huo, Josep Borell ametumia maneno makali kulikosoa shambulizi la Iran dhidi ya Israel akitahadharisha katika ukurasa wake wa X kuhusu mzunguko wa mashambulizi hatari yanayopitiliza mipaka, akiongeza kuwa EU umejitolea kikamilifu na kwa dhati kuepusha vita vya kikanda.

Wakati hayo yakiarifiwa, Lebanon ilifungua anga yake baada ya kulifunga mapema jana kufuatia shambulizi la Iran nchini Israel.

Iran imesema mashambulizi hayo makubwa dhidi ya Israel ni kujibu kuuliwa kwa viongozi wa wanamgambo wanaoungwa mkono na serikali ya mjini Tehran, akiwamo kiongozi mkuu wa kundi la Hezbollah nchini Lebanon, Hassan Nasrallah.

Hili ni shambulizi la pili la moja kwa moja la Iran dhidi ya Israel bada ya jingine la makombora na droni Aprili, mwaka huu kujibu hujuma ya kutokea angani ya Israel katika ubalozi mdogo wa Iran mjini Damascus nchini Syria. **REUTERS, AFP**



Watu wakijificha kando ya barabara mjini Tel Aviv baada ya king'ora kulia kufuatia shambulizi la Iran jana. **PICHA: REUTERS**

## IMF kufanya tathmini ufisadi Kenya

**NAIROBI,** Kenya

WADAU wakuu kwenye Shirika la Kimataifa la Fedha (IMF), wameisihi Kenya itoe ombi kwa IMF la kuchunguza madai ya ufisadi na utalawa mbaya, kama hatua ya kuelekea kupata mikopo iliyokwama kufuatia kusitishwa kwa mswada wa fedha uliolenga kuongeza kodi.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Reuters, mkopo wa takriban dola milioni 600, (Sh. Trilioni 1.6) chini ya mpango wa IMF, na ambao muda wake unamalizika mwaka ujao, umekwama tangu serikali ilipositisha mpango wa kukusanya dola bilioni 2.7 kupitia kodi, kutokana na maandamano ya kitaifa.

Maandamano hayo yalioongozwa na vijana na ambayo zaidi ya watu 50 waliuawa yalifichua madai ya ufisadi, pamoja na utawala mbaya, huku vijana wakilalamika kuwa kodi zao zilitumiwa na wanasiasa kuishi maisha ya kifahari.

Kutokana na hoja hizo za waandamanaji serikali za mataifa ya magharibi zimekuwa zikishinikiza kufanyika kwa tathmini ya IMF kuhusu madai hayo.

Wizara ya Fedha ya Kenya haijasema lolote kuhusiana na ripoti hiyo. Na kwamba tangu 2014, IMF imefanya tathmini kwenye mataifa 14 yakiwamo Ukraine, Cameroon na Sri Lanka. **VOA**

**Maandamano hayo yalioongozwa na vijana na ambayo zaidi ya watu 50 waliuawa yalifichua madai ya ufisadi...**

## Daktari kizimbani tuhuma za mauaji

**KIGALI,** Rwanda

DAKTARI ambaye ni raia wa Rwanda Eugene Rwamucyo (65) anayetuhumiwa kwa mauaji ya halaiki miongo mitatu iliyopita baada ya mauaji ya Watutsi wa nchini humo, amefunguliwa mashtaka huko Paris Ufaransa ili kujibu juu ya tuhuma hizo.

Ilielezwa kuwa Rwamucyo anatuhumiwa kusaidia mamlaka ya nchi yake katika kueneza propaganda dhidi ya Watutsi na kushiriki katika mauaji ya halaiki katika jaribio la kuharibu ushahidi wa mauaji ya halaiki.

Daktari huyo ambaye alifanya kazi ya udaktari nchini Ufaransa na Ubelgiji baada ya kuondoka nchini mwake, alishtakiwa kushiriki katika mauaji ya halaiki, uhalifu dhidi ya binadamu na njama ya kuandaa uhalifu huo, na kwamba endapo atapatikana na hatia anaweza kuhukumiwa kifungo cha maisha jela.

Ilibainishwa kuwa kesi ya Rwamucyo ni ya nane nchini Ufaransa kuhusiana na mauaji ya kimbari mwaka 1994, wakati inakadiriwa watu 800,000 wengi wao wakiwa kabila la Watutsi waliuawa.

Kwa mujibu wa waendesha mashtaka, wanaomtuhumu kwa kueneza propaganda dhidi ya Watutsi Rwamucyo, ambaye alikulia katika familia ya Wahutu, alifuatwa na wapiganaji wanaopinga Watutsi mwishoni mwa miaka ya 1980 baada ya kurejea kutoka masomoni nchini Russia.

Aidha, mwendesha mashtaka alisema, akinukuu taarifa za mashahidi kwamba mtuhumiwa alipokuwa akifundisha chuo kikuu, pia alishiriki katika mauaji ya wagonjwa waliojeruhiwa na kusaidia kuwazika katika makaburi ya halaiki katika jitihada za mwisho za kuharibu ushahidi wa mauaji ya kimbari.

Wakili wake, Philippe Meilhac, alisema Rwamucyo anakanusha kufanya makosa yoyote na anadai kuwa mashtaka hayo yanatokana na upinzani wake kwa serikali ya sasa ya Rwanda.

Wakili huyo alisema ushiriki wake katika kuzika miili katika makaburi ya halaiki ulichochewa na nia ya kuepuka shida ya kiafya ambayo ingetokea ikiwa wangeachwa hadharani. **TRT**

# KINARA WA MABAO LIGI KUU, APAGAWA KUITWA TAIFA STARS

Na Adam Fungamwango

KINARA wa mabao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Selemani Mwalimu, kutoka Fountain Gate, amesema ilikuwa ni ndoto yake kubwa sana kuichezea timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars, lakini hakutegemea kuitwa mapema kiasi hiki.

Akizungumza baada ya mchezo wa Ligi Kuu kati ya timu yake dhidi ya Prisons uliochezwa juzi, Uwanja wa Sokoine, Mbeya timu yake ikifungwa mabao 3-2, lakini mwenyewe akipachika kwa mara nyingine bao moja na kufikisha matano akiwa juu ya orodha ya wafungaji mabao, Selemani alisema anashukuru sana kuchaguliwa kuichezea Stars.

"Yalikuwa malengo yangu makubwa siku moja niitwe kwenye kikosi cha timu ya taifa, Mungu amesikia maombi yangu, leo ni mmoja wa wachezaji 23 walioitwa kunda kikosi cha Stars, ingawa mimi mwenyewe sikutegemea kama nitaitwa mapema kiasi hiki, kusema kweli imenipa faraja sana na naahidi nitalitumikia taifa kwa nguvu zangu zote," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa KVZ ya Zanzibar.

**Jumanne iliyopita, Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Suleiman 'Moroco', alitangaza majina ya wachezaji 23 watakaoingia kambini kesho kwa ajili ya michezo miwili ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za AFCON dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.**

Kuhusu kuwania kiatu cha dhahabu msimu huu, mshambuliaji huyo alisema ni mapema mno kutabiri jambo hilo.

"Ni mapema sana, unajua kwa sasa ninachofanya nikuizoea kwanza Ligi ya Tanzania Bara, lakini pia nafanya hivi ili kuisaidia timu yangu ya Fountain Gate, Ligi bado ngumu na yenye ushindani sana, ni ngumu kutabiri," alisema.

Selemani, alikuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu Zanzibar msimu uliopita akipachika mabao 20, na kutoa 'asisti' saba kwenye michezo 27 aliyocheza.

KIKAPU...




Mchezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya Polisi, Hamad Alli (katikati), akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wa Anmache, katika michuano ya mchezo huo inayoendelea kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Furahisha amtishia 'nyau' Mazombe

Na Shufaa Lyimo

BONDIA Hamadi Furahisha wa Dar es Salaam, amesema ana kila sababu ya kushinda pambano lake dhidi ya Ally Mazombe kutoka Morogoro kutokana na maandalizi yake.

Mabondia hao watapanda ulingoni Oktoba 25 katika ukumbi wa Tanzanite mjini Morogoro kwenye pambano lililopewa jina la ' Homa ya SGR'.

Akizungumza na Nipashe jana wakati akiendelea na maandalizi yake jijini Dar es Salaam, Furahisha alisema ameshawapiga mabondia wa Morogoro hivyo mpinzani wake huyo asubiri kichapo kutoka kwake.

"Kwa mazoezi ninayoendelea kuyafanya nina matumaini makubwa ya kuibuka na ushindi, siku hiyo ninaomba wadau na mashabiki wangu waje kwa wingi kushuhudia kichapo nitakachompa," alisema Furahisha.

Alisema amefanya maandalizi ya muda mrefu ili aweze kutimiza malengo yake siku hiyo kwa kumchakaza mpinzani wake ndani ya raundi ya kwanza tu.

Kwa upande wake kocha wa bondia huyo, Haji Pera alisema kutokana na mazoezi aliyompa, mpinzani wake akae sawa na ajipange.

"Kazi zetu zinaeleweka, huwa hatuna kazi mbovu tunamshukuru Meja Selemani Semunyu kwa kutuandalia pambano hili," alisema Pera.

Kocha huyo aliweka wazi kuwa licha ya mpinzani wao kuwa nyumbani kwao, hawamwogopi na kuahidi kumpa kichapo kikali mbele ya mashabiki wake na wana Morogoro.



# Nuru Mollel akaribia ubingwa gofu

Na Beatrice Shayo

MCHEZAJI wa kulipwa wa mchezo wa gofu, Nuru Mollel anakaribia kutwaa ubingwa wa mashindano ya gofu ya 'Lina PG Tour' yanayofanyika mjini Moshi baada ya kuibuka na ushindi kwenye mizunguko minne kati ya mitano ya michuano hiyo.

Mollel ambaye ni mchezaji wa klabu ya Arusha Gymkhana, amejiweka katika nafasi nzuri ya kuwa bingwa wa michuano hiyo inayochezwa kwa mizunguko mitano ambapo mzunguko wa mwisho unatarajiwa kuchezwa mwezi ujao.

Endapo atafanikiwa kuibuka bingwa wa jumla, atakata tiketi ya kushirki mashindano ya kimataifa ya Dubai baadaye mwaka huu.

Tishio kubwa la Mollel katika kutwaa ubingwa huo lipo kwa mchezajimwenzake, Fadhyl Nkya wa Dar es Salaam ambaye alimaliza wa pili katika mchuano huo.

Katika mzunguko huo wa kwanza Mollel na Nkya walifungana kabla ya mshindi kuamuliwa kwa mashimo ya nyongeza.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mzunguko wa nne wa mashindano hayo, Mollel alisema kuwa bado ni vigumu kuwa na uhakika wa ushindi kwa sababu lolote linaweza kutokea katika raundi ya tano ambayo ni ya mwisho itakayofanyika jijini Dar es Salaam mwezi ujao.

"Upinzani bado ni mkubwa wachezaji wote wanajituma sana ila nitaendelea na mazoezi ili kuhakikisha nafanya vizuri katika raundi ya tano ambayo itafanyika Dar es Salaam," alisema Mollel.

Mollel alisema anatoa ushindi wake huo kwa mdhamini wa mashindano mbalimbali ya gofu na aliyewahi kuwa mwenyekiti wa Chama cha Gofu Nchini (TGU) na Mwenyekiti wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Dioniz Malinzi, kama shukrani kwake baada ya kumsaidia yeye na wenzake kuwa wacheza gofu.

"Nautoa ushindi wangu kwa Malinzi kwa sababu yeye ndiye aliyetupika na kuiva barabara kabla ya kuichezea timu yetu ya taifa na baadaye kuwa wachezaji wa kulipwa," alisema Mollel.

Elisante Lembris ni mcheza gofu wa kulipwa kutoka Arusha alisema naye anamshukuru Malinzi kwa kutumia muda na fedha zake kuwasaidia wazawa na kuwaendeleza wacheza gofu chipukizi ambao miaka 20 baadaye wamekuwa ndiyo vinara wa mchezo huo hapa nchini kwa upande wa wachezaji wa kulipwa.

HABARI MICHEZO

ZISIKUPITE

## ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL iko tayari kuchuana na Manchester United kwa ajili ya kumnunua mlinzi wa kati wa Everton, Jarrad Branthwaite na inaweza kumnunua Muingereza huyo mwenye umri wa miaka 22 ifikapo Januari. ***(Mail)***

## DYCHE KUPEWA FUNGU

KOCHA Sean Dyche atapewa fedha za kuboresha kikosi cha Everton ifikapo Januari mara tu kundi la Friedkin litakapomaliza kuitwaa klabu hiyo na hakuna wachezaji wakubwa watakaouzwa. ***(Football Insider)***

## SOUTHGATE ATAJWA UNITED

KOCHA wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Gareth Southgate ndiye mteule bora wa Manchester United kuchukua nafasi ya Erik ten Hag, imetajwa. ***(ipaper)***

## ALLEGRI KUMRITHI TEN HAG

MANCHESTER United pia imeonyesha nia ya kuzungumza na kocha wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri iwapo watamfuta kazi, Erik Ten Hag. ***(Football Insider)***

## KLOPP AIKATAA UJERUMANI

KOCHA wa zamani wa Liverpool, Jurgen Klopp, amepuuzilia mbali uvumi kuwa atachukua nafasi ya kocha wa timu ya taifa ya Ujerumani. ***(Mail)***

## INIESTA AKARIBIA KUSTAAFU

KIUNGO wa kati wa zamani wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Andres Iniesta, mwenye umri wa miaka 40 anatarajiwa kutangaza kustaafu soka siku zijazo. ***(Goal)***

## EDERSON KUMRITHI RODRI

KIUNGO wa kati wa Crystal Palace na England, Adam Wharton, mwenye umri wa miaka 20, na kiungo wa kati wa Atalanta na Brazil, Ederson (25), wako kwenye orodha ya Manchester City ili kuziba pengo la Rodri (28), ambaye ni majeruhi. ***(Caught Offside)***

## GORDON MAMBO SAFI

WINGA wa England, Anthony Gordon mwenye umri wa miaka 23, anatazamiwa kusaini mkataba mpya wa kuendelea kusalia Newcastle United hadi mwaka 2030. ***(Fabrizio Romano)***

## WILSON APEWA RUHUSA

KLABU ya Newcastle United iko tayari kumruhusu mshambuliaji wa England, Callum Wilson, mwenye umri wa miaka 32, kuondoka bila malipo msimu ujao iwapo hawatapata mbadala wake Januari. ***(Give me Sport)***

## YAZICI KUTUA OLYMPIAKOS

MSHAMBULIAJI wa Uturuki, Yusuf Yazici, mwenye umri wa miaka 27 anatazamiwa kusaini mkataba wa miaka mitatu na klabu ya Ugiriki ya Olympiakos baada ya kuondoka katika klabu ya Lille ya Ufaransa. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




**LONDON,** England

BUKAYO Saka alisema "huu ni mwaka" kwa Arsenal kuwa washindi baada ya kufunga mabao 2-0 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Paris Saint-Germain iliyochezwa kwenye Uwaja wa Emirates hapo juzi.

**Kikosi cha Kocha Mikel Arteta kilipanda katika nafasi ya nane bora ya jedwali jipya la Ligi ya Mabingwa, ambayo inawahakikishia nafasi ya kufuzu kwa hatua ya 16 baadaye msimu huu, kwa mabao ya Kai Havertz na Saka dhidi ya mabingwa hao wa Ufaransa.**

### ●●● Nyota huyo wa Arsenal amesema huu mwaka wao na...

Washikabunduki hao wamemaliza nyuma ya Manchester City kwenye Ligi Kuu England katika misimu miwili iliyopita na hawajashinda taji lolote kubwa tangu kubeba Kombe la FA msimu wa 2019-20, lakini baada ya ushindi huo wa kujiamini dhidi ya PSG, Saka alisema: "Arsenal sasa inakuwa timu ambayo inaweza kushinda medali, taji na "ana njaa" ya kwenda hatua ya mwisho ya kupata mafanikio.

"Sitaki kuweka shinikizo kubwa kwetu, lakini nadhani huu ni mwaka wetu," alisema Saka.

"Tumekuwa karibu miaka miwili iliyopita na tunakaribia zaidi. "Msimu huu, kuna njaa nyingi kwangu. Miaka ya nyuma, tulikuwa mshindi wa pili. Ni roho tu iliyo ndani yangu kwamba nataka kushinda msimu huu na bila shaka, ninajiamini sana. Pamoja na mambo hayo mawili, inasaidia.

"Tunajiamini, tunaamini sisi ni timu ya juu. Tumeonesha hilo usiku wa leo (juzi) dhidi ya PSG."

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta aliunga mkono maoni ya Saka kwa kusema ni muhimu kwa timu yake kushinda kikosi kikubwa cha Ulaya, PSG.

"PSG ni moja ya timu bora duniani hivyo kuzifunga, kunaongeza imani tunaweza kushindana na timu yoyote katika ngazi yoyote," alisema Arteta.



# FERNANDES AFUTIWA KADI NYEKUNDU

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United ilishinda rufani yao dhidi ya kadi nyekundu ya Bruno Fernandes wakati wa kichapo cha mabao 3-0 walichopata kutoka kwa Tottenham Hotspur Jumapili iliyopita.

Fernandes alitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumchezea rafu, James Maddison, kipindi cha kwanza.

Nahodha huyo wa United alionekana kuteleza na kutua kwenye mguu wa Maddison. Mwamuzi, Chris Kavanagh, alimwonyesha Fernandes kadi hiyo ya moja kwa moja, na uamuzi huo uliungwa mkono na VAR chini ya mwamuzi, John Brooks.

Lakini baada ya United kukata rufani mapema Jumatatu, FA ilithibitisha wamebatilisha uamuzi huo. Fernandes ataepuka kufungiwa na atakuwapo kwa mechi tatu zijazo za Ligi Kuu England dhidi ya Aston Villa, Brentford na West Ham.

Taarifa ya FA iliyotolewa jana ilisomeka: "Bruno Fernandes atakuwapo kwa mechi tatu zijazo za Manchester United baada ya kufutwa kadi nyekundu aliyoonyeshwa."

Kocha wa United, Erik ten Hag alisema kadi nyekundu "ilibadilisha mchezo" dhidi ya Tottenham licha ya kuwatazama wageni wakitawala hata kabla ya Fernandes kutolewa.

Fernandes alikasirishwa na uamuzi huo na kudai Maddison mwenyewe alisema haikuwa kadi nyekundu.

"Nadhani machoni pa kila mtu, unaweza kuona hiyo sio kadi nyekundu, kwa sababu kama hii ni kadi nyekundu nadhani tunapaswa kuangalia matukio mengine mengi," alisema Fernandes.

# Enrique alia nyota PSG wamekosa ari



**LONDON,** England

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Luis Enrique, amesema hajui itachukua muda gani kurejesha timu yake katika ubora baada ya kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Arsenal kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mabingwa hao wa Ufaransa, ambao walimpoteza Kylian Mbappé aliyejiunga na Real Madrid msimu wa joto na kuonekana kama timu ya mpito, walipata kipigo chao cha kwanza msimu huu.

Mabao ya Kai Havertz na Bukayo Saka yaliiweka Arsenal uongozini kabla ya kipindi na ingawa PSG waligonga mwamba mara mbili lakini hawakupata bao.

Enrique, ambaye alimwacha nje mshambuliaji Ousmane Dembélé kwa sababu za kinidhamu, alikubali jukumu lake la kushindwa, lakini alionekana kutilia shaka ari ya wachezaji wake.

"Leo (juzi) tulikuwa mbali na viwango unavyohitaji katika mechi ya aina hii. Arsenal walikuwa bora zaidi kwa shinikizo, nguvu, walishinda kila pambano," alisema Enrique akiwaambia waandishi wa habari.

"Haiwezekani kucheza kwa matokeo chanya wakati hutashinda pambano lako lolote uwanjani, mabeki wao waliwatarajia washambuliaji wafunge."

Mhispania huyo aliiongoza PSG kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita walipoishinda klabu yake ya zamani ya Barcelona katika robo fainali huku Mbappé akifunga mara mbili.

"Siwezi kutathmini vizuri kiwango cha timu yetu, itabidi tusubiri hadi mwisho wa msimu," alisema.

"Huyu alikuwa mpinzani wetu mkubwa wa kwanza katika kiwango cha juu zaidi. Tulijua tangu dakika ya kwanza wangetukandamiza na walifanya hivyo na hatukuweza kustahimili shinikizo hilo."

## De Jong afurahia kurejea uwanjani

**BARCELONA,** Hispania

FRENKIE de Jong alirejea Barcelona ambayo ilikuwa inasubiriwa kwa muda mrefu Jumanne baada ya kuwa nje ya uwanja kwa takriban miezi mitano kwa sababu ya jeraha la kifundo cha mguu.

Kiungo huyo Mholanzi alichukua nafasi ya Lamine Yamal dakika ya 75 katika ushindi wa mabao 5-0 ambao Barcelona walipata dhidi ya Young Boys kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

De Jong aliumia kifundo cha mguu wake wa Aprili katika mechi ya Ligi Kuu Hispania Clasico dhidi ya Real Madrid. Pia alikosa kucheza Euro kwa sababu ya jeraha hilo.

Kukaa kwa muda mrefu benchi kulisababisha kutendewa vibaya na vyombo vya habari vya ndani, ambavyo vilitilia shaka ratiba yake ya kupona na kiasi cha fedha anachopata, na De Jong alikiri kabla ya kurejea kwake kwamba muda wa mapumziko na baadhi ya ripoti kuhusu jeraha lake zilikuwa na madhara.

"Nimefurahishwa sana na ushindi na kurejea kucheza," alisema De Jong baada ya mchezo huo.

"Mashabiki walinipokea vizuri na nashukuru kwa hilo kwa sababu huwezi jua utapokelewa vipi, sikutarajia, nimefurahishwa na jinsi nilivyokaribishwa.

"Timu iko katika hali nzuri na imekuwa tangu kuanza kwa msimu huu. Tunacheza vizuri, inabidi tuendelee sasa, tuendelee kuimarika na kuona ni wapi inatufikisha."

Alipoulizwa ni kwa jinsi gani alijiona anafaa katika timu ya Kocha, Hansi Flick na kama angekuwa tayari kwa nafasi kutoka benchi la wachezaji wa akiba, Mholanzi huyo alisema atacheza wakati wowote na popote atakapopangiwa.

"Inategemea na kocha. Anachagua timu na nani anacheza na nitatoa kila niwezalo," alisema De Jong.



# YANGA PRINCESS, JKT QUEENS FAINALI NGAO YA JAMII

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Wanawake, Yanga Princess jana ilifanikiwa kutinga fainali ya Ngao ya Jamii baada ya kuifunga Simba Queens kwa mikwaju ya penalti 4-3 katika mchezo wa nusu fainali uliochezwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

**Timu hizo zililazimika kwenda kwenye matuta baada ya kumaliza dakika 90 zikifungana bao 1-1, huku Simba Queens ikisawazisha bao dakika za mwisho za mchezo kupitia kwa Jentrix Shikangwa.**

Shujaa katika mchezo wa jana alikuwa kipa, Rita Akarekor anayeichezea pia timu ya taifa ya Nigeria akiwa amesajiliwa msimu huu kutoka klabu ya Delta Queens ya nchini humo, aliyeokoa penalti tatu za wachezaji wa Simba Queens, Ester Mayala, Vivian Corazone na Fatma Issa.

Penalti nne za Yanga zilifungwa wavuni na Danai Bhobho, Anges Palyango aliyefunga bao la kwanza kwa Yanga ndani ya dakika 90, Uzoamaka Igwe, na Diana Antwi, huku Wema Richard, na Neema Paul wakikosa.

Simba Queens, penalti zao zilifungwa na Shikangwa, Precious Christoper na Asha Djaffar.

Kwa matokeo hayo, Yanga Princess itakutana na JKT Queens katika mchezo wa fainali, utakaochezwa Jumamosi kwenye uwanja huo huo.

Kabla ya mchezo huo, JKT Queens iliichakaza Ceasiaa Queens katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali hiyo, ikiwa ni ishara ya kuanza kwa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa wanawake.

Yanga Princess ilianza mchezo huo kwa kasi, kwani sekunde ya 28 tu walikuwa wameshafika langoni kwa wapinzani wao ambapo shuti la Rebeca Ajimuda lilipanguliwa na kipa Jeneth Shija na kuwa kona iliyozaa bao.

Ilikuwa ni dakika ya kwanza tu ya mchezo wakati kona iliyopigwa na Silvia Thomas, ilimkuta, Agness Palangyo ambaye alijaza wavuni kwa kichwa mbele ya msululu wa mabeki wa Simba Queens ambao walikuwa wamesimama tu.

Baada ya hapo ni kama wachezaji wa Simba Queens walichanganyikiwa kwa bao hilo la mapema kwani wakawapa nafasi wapinzani wao kutawala pambano na kufanya mashambulizi kadhaa ambayo hata hivyo hayakuwa ya hatari sana.

Yanga Princess ikiwa na wachezaji wengi wapya iliyowasajili msimu huu, ilionekana kubadilika kabisa tofauti na ile ya msimu uliopita hasa winga wake wa kushoto, Rebeca ambaye alikuwa akichachafya ngome ya Simba Queens.

Katika hali isiyo ya kawaida na ya kushangaza kikosi cha Simba Queens ikilianza bila wachezaji wake tegemeo kama Elizabeth Wambui, Shikangwa, Corazone, Djaffar na Precious Christoper, ambao waliingia dakika 15 za mwisho kabla ya kipindi cha kwanza baada ya mambo kuonekana kuwa mazito.

Baada ya kuingia kwa wachezaji Simba ilibadilika kiuchezaji na kuanza kuishambulia Yanga na kucheza soka lao lililozoeleka.

## Makata afurahia ushindi wa kwanza Prisons

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Tanzania Prisons, Mbwana Makata, ameeleza kufurahishwa na ushindi wa kwanza kwa timu yake kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kucheza michezo sita sawa na dakika 540, akisema huo ni mwanzo tu wa mazuri ambayo yanakuja kwenye timu yake.

Awali Prisons ilicheza dakika 450 bila kupata ushindi, ikiwa ni michezo mitano, ikitoa sare nne na kupoteza mmoja, kabla ya juzi kupata ushindi wa kwanza wa mabao 3-2, dhidi ya Fountain Gate, ikicheza uwanja wake wa nyumbani, Sokoine jijini Mbeya.

Makata, alisema haikuwa rahisi, kwani walikuwa wakitanguliwa kufungwa, lakini mara zote mbili walifanikiwa kusawazisha na hatimaye kupata bao la ushindi.

"Niwapongeze wachezaji wangu, wamepambana kwa kila njia, walicheza wakiwa na uchovu mkubwa kwani tulitoka safarini Ruangwa kucheza na Namungo, katika mchezo huu haikuwa rahisi kushinda kwa sababu tulitanguliwa mara mbili.

Nasema hivi kwa sababu Fountain ni timu ngumu, ina washambuliaji wazuri ambao ukifanya kosa moja wanaweza kukuadhibu," alisema kocha huyo.

Hata hivyo alisema amegundua udhaifu sehemu ya ulinzi kiasi cha kuruhusu mabao mawili ambayo kwa upande wake alisema yalikuwa rahisi sana, hivyo anakwenda kulifanyia kazi.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Fountain Gate, Mohamed Muya, aliwapongeza wapinzani wake kwa ushindi na kuwapa pole viongozi, wachezaji na mashabiki wa timu yake.

"Niipongeze timu iliyoshinda, walikuwa kwenye kiwango bora, nawapa pole viongozi, wachezaji wangu na mashabiki waliotoka Manyara kuja Mbeya kushangilia timu yao," alisema kocha hiyo.

Mabao ya Prisons kwenye mchezo huo yalifungwa na Nurdin Choma kwa mkwaju wa penalti, Ezekia Mwashilindi na Vedastus Mwihambi, huku ya Fountain Gate yakifungwa na Selemani Mwalimu na Kassim Selemani.

Matokeo hayo yanaifanya Prisons kufikisha pointi saba katika michezo sita iliyocheza ikiwa kwenye nafasi ya tisa, Fountain Gate inasalia na pointi zake 13, ikiwa kwenye nafasi ya pili kwenye msimamo.



Balozi wa Heshima wa Brazil, Zanzibar, Abdulsamad Abdulrahim, akimkabidhi Sh. 500,000, Mudrik Hamid, mshindi wa pili katika michuano ya mashindano ya 'Zanzibar Body Builder', kumtafuta 'Mr. Zanzibar'. Mchango huo ni ahadi yake ya kusaidia kuhamasisha na kuleta mabadiliko kwa vijana kwa ajili ya maendeleo ya sekta ya michezo na kujiepusha na matumizi ya dawa za kulevya. **PICHA: HISANI YA BALOZI**

## *Gamondi aandaa mkakati kuimaliza Pamba Jiji FC*

INATOKA UK. 24

Tutaingia kwa kuwaheshimu Yanga kwani ni moja ya timu bora nchini, sisi pia tumejiandaa kukabiliana nao, tutajitahidi kucheza mpira mzuri ili tupate matokeo mazuri," alisema Mkanwa ambaye atakuwa kwenye benchi kwa mara ya kwanza kusaidiana na Goran Copunovic baada ya kujiunga na timu hiyo akitokea Biashara United ya Mara.

Pamba Jiji ipo nafasi ya 14, imecheza michezo sita, imetoka sare nne na kupoteza michezo miwili na imekusanya pointi nne.

## Simba yaiandalia Coastal dozi

INATOKA UK. 24

Kikosi cha Simba, jana kilianza mazoezi yake rasmi kujiandaa na mchezo huo, baada ya mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara kati yake na Dodoma Jiji uliochezwa Jumapili iliyopita, Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

"Kikosi kinaanza mazoezi leo (jana), kuelekea katika mchezo huo, baada ya kutoka Dodoma tulikuwa tunafanya mazoezi mepesi mepesi tu kwani tangu tutoke Libya kucheza na Al Ahli Tripoli vijana hawakupumzika, kocha akaamua kuwapumzisha kwa kuwapa mazoezi ambayo si magumu, lakini leo mazoezi rasmi ndiyo yanaanza," alisema.

Simba haijafungwa mchezo wowote wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union tangu msimu wa 2019/20, ikiwa imecheza michezo 12, ikishinda michezo 10 na sare mbili.

Michezo

Alhamisi Oktoba 3, 2024

Nipashe



De Jong afurahia kurejea dimbani UKURASA 22

# GAMONDI AANDAA MKAKATI KUIMALIZA PAMBA JIJI

●●● Asema ameifuatilia timu hiyo katika michezo yake na kugundua ni...

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amesema tayari ameandaa mpango mkakati wa kuhakikisha wanaibuka na ushindi kwenye mchezo wa leo dhidi ya Pamba Jiji Fc huku akitamba kuwa ameifuatilia vya kutosha timu hiyo.

**Gamondi, amesema licha ya wapinzani wao hao kutopata ushindi kwenye mchezo wowote katika ligi mpaka sasa bado wana uimara mkubwa kwenye safu yao ya ulinzi hivyo ni lazima wajipange vizuri kutafuta njia ya kupata mabao.**

Yanga leo itashuka kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kucheza na timu hiyo mchezo ambao utaanza saa 12:30 jioni.

Kocha huyo raia wa Argentina, amesema ameifuatilia sana timu hiyo na kugundua mambo kadhaa ambayo ameyafanyia kazi kabla ya kukutana nao leo.

"Najua imepanda daraja msimu huu, haijashinda mechi yoyote kati ya sita ambazo imecheza, lakini imeruhusu mabao matano tu katika michezo hiyo, lakini kwa sababu inacheza na Yanga, haitokuja kucheza kama inavyocheza na timu nyingine, watataka kushinda, watataka kurudi kwenye njia, hivyo natarajia mchezo utakuwa mgumu kwani imeonyesha kuwa hairuhusu mabao, ni timu ngumu kufungika, ina mabeki wazuri," alisema Gamondi.

Hata hivyo alisema wameandaa mpango wa kuhakikisha wanawafungua mabeki wa Pamba Jiji na kutengeneza nafsi za kufunga ambapo amewataka washambuliaji wake kuzitumia vizuri kila nafasi watakayoipata.

"Tutajaribu kadri tunavyoweza, tumecheza michezo kama minne hivi mfululizo, wachezaji wangu wamechoka, hivyo haitokuwa rahisi kushinda, lakini tupo tayari, tumeandaa mkakati mzuri ili tupate pointi tatu muhimu," alisema kocha huyo.

Yanga inaingia katika mchezo huo ikiwa kwenye nafasi ya nne katika msimamo, ikikusanya pointi tisa kwa michezo mitatu iliyocheza, imeshinda michezo yote na kufanikiwa kufunga mabao manne bila wenyewe kuruhusu bao lolote.

Kwa upande wake, akizungumzia mchezo huo wa leo, Kocha Msaidizi wa Pamba Jiji, Henry Mkanwa, amesema yeye na wachezaji wake hawana presha kabisa na mchezo huo na wataingia kucheza kama walivyofanya kwenye michezo mingine iliyopita, lakini wataongeza umakini zaidi.

"Sina presha mimi na vijana wangu. Sisi tunakwenda kucheza mpira, tutashambulia na kuzuia kwa wakati mmoja.

INAENDELEA UKURASA 23



Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi

## Simba yaiandalia Coastal dozi nene

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa klabu ya Simba umesema wanaamini kocha wa timu hiyo, Fadlu Davids, amekiandaa vizuri kikosi chao kuhakikisha wanatoa dozi kubwa kwenye mchezo wa kesho dhidi ya Coastal Union.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema kocha pamoja na kuridhishwa na kiwango cha uchezaji wake, lakini hajaridhishwa na utumiaji nafasi katika michezo miwili ya mwisho dhidi ya Azam FC na Dodoma Jiji.

Ahmed, amesema kocha Fadlu anataka wachezaji wake watumie nafasi zinazopatikana hasa kipindi cha kwanza ili kuifanya mechi kuwa rahisi na isiyo na presha kipindi cha pili.

"Tuna kazi ya kumwonyesha Coastal Union kuwa hii ni Simba mpya kwa kumwandalia dozi nene, kocha anataka nafasi zinazopatikana zitumiwe kwa ukamilifu, katika michezo yetu miwili dhidi ya Azam FC na Dodoma Jiji ameona mapungufu kwani mpaka kipindi cha kwanza kinamalizika katika mechi hizo, Simba tulitakiwa tuwe mbele hata kwa mabao matatu au manne, kwa hiyo kazi yake ni kurekebisha hilo ili Wagosi wa Kaya wawe mfano," alisema.

Hata hivyo, amesema haitokuwa mechi rahisi kama wachezaji wao hawatopambana kwani mara nyingi Coastal Union huwa ni wabishi wanapocheza dhidi ya Simba.

"Itakuwa mechi ngumu, kila mtu anahitaji pointi tatu, haitokuwa nyepesi kwa upande wowote ule, ila sisi tumejipangia kumaliza mechi tano za mwanzo kwa ushindi, tumeshinda nne, bado moja ili kukamilisha robo ya malengo tuliyojiwekea na kama tukifanikiwa hilo yatakuwa maendeleo makubwa kwetu," alisema Ahmed.

INAENDELEA UKURASA 23

## *Yanga Princes, JKT fainali Ngao ya Jamii* UK.23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >